MADA: UUNDAJI WA NOMINO KATIKA KISWAHILI

NA: ESTHER MUNGUTI

"Tasnifu hii imetolewa ili kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya "Master of Arts" katika chuo kikuu cha Nairobi".

1989

UNIVERSITY OF NAIROBI LIBRARY
0145012 1

## U N G A M O

"Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kingine chochote".

Munguti

ESTHER MUNGUTI
(Mtahiniwa)

"Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa kazi hii wa chuo kikuu".

DKT. JAY KITSAO

DKT. MOHAMED BAKARI

## YALIYOMO


UKURASA

Ungamo

Yaliyomo (i)

Shukrani (iii)

Muhtasari (iv)

SURA YA KWANZA

1.0 Utangulizi 1

1.1 Somo la Utafiti 1

1.2 Madhumuni ya Tasnifu 2

1.3 Sababu za Kuchagua Mada hii 3

1.4 Yaliyoandikwa kuhusu Mada hii 5

1.5 Upeo wa tasnifu 16

1.6 Msingi wa Nadharia 17

1.7 Njia za Utafiti 18

Tanbihi 20

SURA YA PILI

2.0 Utangulizi 21

2.1 Fonolojia ya Kiswahili 21

2.2 Mofolojia ya Kiswahili 32

2.3 Unyambuaji 38

2.4 Utumiaji wa Viambisho 40

2.5 Dhana ya Uambishaji 56

2.6 Kubadili Kategoria 59

2.7 Kimalizio 62

Tanbihi 64

SURA YA TATU

3.0 Nomino za Mkopo 65

3.1 Utangulizi 65

3.2 Mabadiliko yanayokumba nomino zilizokopwa 70

3.3 Utohozi 80

3.4 Kaleki 85

3.5 Akronimu 88

3.6 Kimalizio 92

Tanbihi 94

SURA YA NNE

4.0 Utangulizi 95

4.1 Maneno ambatano 95

4.2 Aina za maneno ambatano 98

4.3 Taratibu ndogondogo 101

4.4 Uradidi 101

4.5 Mafungu ya a- unganishi 103

4.6 Uhamishaji wa maana 103

4.7 Utumiaji wa fonimu za lugha 104

4.8 Matumizi ya kompyuta 104

4.9 Kuhusisha dhana na kitajwa 106

4.10 Uundaji wa Kibinafsi 106

4.11 Ukatizaji 107

4.12 Kimalizio 108

Tanbihi 109

SURA YA TANO

5.0 Hitimisho 110

Marejeo 113

## SHUKRANI

Kwanza ningependa kuwashukuru wasimamizi wangu Dkt. Kitsao na Dkt. Bakari kwa msaada wao uliowezesha kazi hii kufanikiwa. Vile vile natoa shukrani zangu za dhati kwa wahadhiri wengine wa idara ya Isimu na Lugha za Kiafrika hususa Prof. Mutahi, Dkt. Okombo na Mwalimu Kazungu Kadenge kwa mchango wao kuhusu Kazi hii.

Pili, nawashukuru wanafunzi wenzangu, Bi Lugano R.S., Habwe J.H. na Njue J.G. ambao walinitia moyo nilipokaribia kukata tamaa.

Tatu, shukrani zangu ziwaendee wazazi wangu Munguti N. na Muthoni M. ambao walielewa kuwa masomo yalinipunguzia nafasi ya kwenda kuwaona mara kwa mara na hawakunilaumu kamwe. Pia nawashukuru ndugu zangu Kiseli na Michael na dada zangu Jane na Ndinda kwa kunipa nafasi niendelee na masomo yangu. Nawashukuru kwa kutonihusisha na matatizo yao ya hapa na pale ili kuepuka kuathiri masomo yangu kwa njia yoyote ile. Vile vile siwezi kumsahau Muthoni 'Junior' ambaye hakuwahi kuelewa ni kwa nini 'shule' yetu haikufungwa ili kuniwezesha kwenda nyumbani kuwaona mara nyingi zaidi.

Mwisho, shukrani zangu ni kwa mpigaji taipu, Mercy N. Kimone.

Kwa wote walionisaidia nasema SHUKRANI.

## MUHTASARI

Katika tasnifu hii tunaangalia njia mbali mbali za uundaji wa nomino katika Kiswahili sanifu.

Sura ya kwanza ni utangulizi wa utafiti. Katika utangulizi huu tumejishughulisha na somo la utafiti, madhumuni ya tasnifu, sababu za kuichagua mada hii, yalioandikwa kuhusu mada hii, msingi wa nadharia na mwishowe njia za utafiti.

Sura ya pili imeanza kwa kutoa muhtasari wa fonolojia na mofolojia ya Kiswahili. Imeendelea kushughulikia taratibu za unyambuaji na uambishaji ambazo zinahusu kwanza, utumiaji wa viambisho na pili, kubadili neno la kategoria moja hivi kwamba linaweza kutumiwa katika kategoria nyingine.

Katika sura ya tatu tumeshughulikia maneno mikopo na tafsiri mikopo. Katika kujadili mikopo hii tumezishughulikia taratibu za utohozi, akronimu na kaleki.

Katika sura ya nne tumeangalia utaratibu wa kuunganisha maneno na taratibu nyingine ndogo ndogo kama vile kurejelea mzizi au uradidi, uhamishaji wa maana, mafungu ya a-unganishi n.k. Vile vile katika sura hii tumeangalia mapendekezo yaliyotolewa na baadhi ya wasomi na wanaisimu kuhusu njia ambazo zinaweza kutumiwa kuunda nomino katika Kiswahili.

Sura ya tano ni hitimisho la utafiti wetu. Katika sura hii tumezijadili kauli muhimu zilizojitokeza katika sura hizo nyingine.

## SURA YA KWANZA

### 1.0. UTANGULIZI

Eneo la msamiati limewavutia wanaisimu na wasomi wingi. Hii ni kwa sababu ya umuhimu wake katika sarufi na ukuzaji wa lugha kwa jumla. Katika sura hii, ambayo ndiyo utangulizi wa utafiti, tutaanza kwa kuangalia somo la utafiti, kisha twende kwenye madhumuni ya tasnifu, sababu za kuichagua mada hii, yaliyoandikwa kuhusu mada hii, msingi wa nadharia na njia za utafiti.

### 1.1. SOMO LA UTAFITI

Tasnifu hii inatarajia kujishughulisha na njia mbalimbali za uundaji wa nomino katika Kiswahili sanifu. Kwa kufanya hivyo inakusudia kueleza taratibu za uundaji wa nomino katika Kiswahili kwa upana na undani zaidi.

Kuna taratibu kadha za kuunda nomino katika Kiswahil Tutatizama taratibu hizi katika makundi matatu. Kundi la unyambuaji na uambishaji, kundi la maneno - mikopo na tafsiri mikopo na hatimaye kundi la maneno ambatano na taratibu nyingine ndogo ndogo.

Hapo awali, kazi zilizoshughulikia uundaji wa nomino katika Kiswahili ziligusia tu taratibu zinazotumiwa bila kueleza kwa undani. Kwa mfano, kauli kuwa 'katika Kiswahili nomino huundwa kwa kutumia mizizi ya vitenzi pekee' (Polome 1967:77) ni kauli inayopotosha. Kazi nyingine zimejishughulisha na uundaji wa maneno kwa jumla na kugusia kidogo tu juu ya uundaji wa nomino kama njia mojawapo ya uundaji wa maneno. Kwa mfano Myachina (1981).

Ni tumaini letu kuwa kazi hii itatoa mwangaza zaidi kuhusu uundaji wa nomino katika Kiswahili na hali kadhalika kusahihisha kasoro kadha zilizojitokeza katika kazi za hapo awali.

## 1.2. MADHUMUNI YA TASNIFU

Katika sehemu ya 1.1, tulitaja kuwa uundaji wa nomino katika Kiswahili sanifu haukushughulikiwa vya kutosha. Ni madhumuni ya tasnifu hii kulitizama swala hili kwa mapana na marefu yake. Katika kufanya hivyo tunanuia kujitokeza na utaratibu bora zaidi wa kulitazama suala hili la uundaji wa nomino katika Kiswahili sanifu.

Pili tunanuia kuzitafiti njia mbalimbali za uundaji wa nomino katika Kiswahili na kujaribu kuona ni njia ipi inayotumika zaidi na ambayo inatoa mchango mkubwa katika uundaji wa nomino.

Tatu, dosari kadha wa kadha zimejitokeza katika tafiti za hapo awali. Ni lengo letu kujaribu kusahihisha makosa na madai yasiyo sahihi. Kwa mfano, ni madhumuni yetu kuchunguza ikiwa ni kweli kuwa mofimu {n} na {zi} hutumiwa kuunda nomino kama tafiti za wasomi kama Polome (1967) na Myachina (1981) zinavyodai. Vile vile ni lengo letu kuonyesha kuwa, hata ingawa nomino nyingi za Kiswahil huundwa kutokana na mizizi ya vitenzi, kwa kutumia mofimu maalum pamoja na viambishi vitangulizi vya ngeli, kuna nomino kadha ambazo huundwa kutokana na misingi ya vivumishi na nomino nyingine kwa mfano ubaya, uzuri na kadhalika.

Nne, tumetaja katika sehemu ya 1.4. kuwa baadhi ya wasomi walioshughulikia uundaji wa nomino au maneno katika Kiswahili wamechukulia unyambuaji na uambishaji kuwa taratibu sawa. Ni madhumuni yetu katika tasnifu hii kuzieleza kwa uwazi taratibu hizi ili msomaji yeyote awe na uwezo wa kuzitofautisha bila kukanganyika.

Tano, kwa kutafiti eneo hili la uundaji wa nomino kwa upana zaidi, tunatarajia kuziweka wazi zaidi taratibu zinazotumiwa ili wasomi wa baadaye wanufaike na pia ziwe rahisi kwa yeyote anayenuia kuunda nomino kufanya hivyo bila matatizo mengi.

## 1.3 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII

Maneno ni muhimu sana kwa sababu ndiyo hasa huunda lugha. Kama anavyoandika Kapinga (1975:44) 'maneno ni majengo ya lugha ambayo hufanya sehemu ndogo ndogo za

za misemo yetu'. Ili lugha ikue ni lazima iwe na njia fulani ya kupanua na kuongeza msamiati wake ili kukabiliana na uvumbuzi wa kisasa na vile vile kuendeleza mawasiliano ya kila siku. Uundaji wa maneno mapya na hasa nomino hutajirisha lugha na kukuza msamiati.

Kando na umuhimu wa uundaji wa nomino katika sarufi na lugha kwa jumla, tulichagua mada hii ili kuishughulikia kwa upana zaidi ya ilivyofanywa hapo awali. Tafiti nyingi zilizofanywa hapo awali zimelifinya[1] swala lenyewe ili kulishughulikia pamoja na uundaji wa maneno ya kategoria nyingine. Ni maoni yetu kwamba swala hili halikupewa uzito unaostahili na ndiyo maana tukaamua kurekebisha upungufu huu.

Vile vile katika kuchunguza utafiti ambao umefanywa katika eneo hili la msamiati, tumegundua kuwa uundaji wa istilahi umeshughulikiwa na unazidi kushughulikiwa zaidi ya uundaji wa msamiati wa kawaida. Ili kukuza msamiati mzima wa lugha kwa jumla na kuwa na maendeleo yanayolingana ni lazima utafiti wa msamiati wa kawaida uende sambamba na ule wa istilahi.

Sababu nyingine iliyotufanya kuchagua mada hii ni kurekebisha makosa kadha wa kadha ambayo yamejitokeza katika tafiti za hapo awali. Kwa mfano tunakusudia kuonyesha kuwa nomino katika Kiswahili haziundwi tu kutokana na mizizi ya vitenzi pekee bali kuna baadhi ya nomino

ambazo huundwa kwa kutumia mizizi ya vivumishi na ya nomino nyingine.

Mwisho, hakuna kazi yoyote yenye uzito iliyofanywa au kuandikwa katika eneo hili la uundaji wa nomino za kawaida kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

## 1.4 YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA HII

Kazi nyingi zilizoandikwa juu ya mada hii zimeishughulikia kwa viwango tofauti tofauti. Nyingi kati ya kazi hizo zimeshughulikia tu baadhi ya taratibu mbalimbali za kuunda nomino lakini hakuna iliyoshughulia taratibu zote kwa kikamilifu.

Moja kati ya kazi ambazo zimetoa mchango mkubwa na wa hali ya juu ni ile ya Myachina (1981). Katika sura aliyoiita 'Msamiati na uundaji wa maneno' amezungumzia juu ya uundaji wa nomino kama njia mojawapo ya uundaji wa maneno kwa jumla. Amesema kuwa nomino katika Kiswahi huundwa kwa kutumia viambisho vitangulizi vya ngeli na viambisho vifuatilizi kama vile {e}, {fu (vu)}, {i} , {o} na {zi(+i)} . Vile vile amesema kuna nomino nyingine ambazo huundwa kwa kuunganisha maneno mawili kwa mfano mwanasheria, au kuhamisha maana kwa mfano nomino kama vile ndege, tawi na mtego au kwa kutumia virai kwa mfano chombo cha kuzimia moto na kitabu cha kuandikia. Njia nyingine ni ya kukopa kutoka lugha nyingine. Anaorodhesha maneno ambayo yamekopwa kutoka , Kiarabu, Kiajemi, Kihindi,

Kijerumani, Kiingereza, Kituruki, na Kireno. Kazi hii itatufaa sana kwa sababu imejaribu sana kueleza nyingi kati ya taratibu zinazotumiwa kuunda nomino katika Kiswahili.

Msomi mwingine aliyetoa mchango mkubwa ni Polome (1967). Polome pia amezungumza juu ya uundaji wa nomino kwa kutumia **viambisho** vitangulizi vya ngeli na viambisho vifuatilizi kama vile {i}, {u}, {o} na {e} . Polome anasema kuwa nomino kuwa nomino hunyambuliwa kutokana na mizizi ya vitenzi pekee. Kuhusu kuunganisha maneno, anasema kuwa nomino iliyonyambuliwa kutokana na mzizi wa kitenzi huongezwa kwenye yambwa tendwa ili kuunda nomino. Kwa mfano mwuzasamaki, kifunga bei na kadhalika. Anaendelea kusema kuwa Kiswahili pia huunganisha maneno kwa kutumia {ana} kwa mfano mwanafunzi, mwanachama na mwanamimba na kwa kutumia kivumishi kuu kwa mfano mkufunzi, mkurugenzi na kadhalika. Vile vile ametaja aina nyingine za kuunganisha maneno kama vile kutumia neno mfanya kwa mfano mfanya-kazi, mfanya-biashara n.k. Mwishowe, anataja urudiaji wa mzizi kama njia mojawapo ya uundaji wa nomino na kutoa mfano wa neno kizunguzungu. Kazi hii itatufaa kw kiasi fulani tu kwani imejikita zaidi upande wa unyambuaji na uambishaji.

Kazi nyingine itakayotufaa sana ni ile ya Quirk, Greenbaum, Leech na Svartvik (1972) katika chapisho lao la pamoja liitwalo A grammar of contemporary English.

Kitabu hiki kina sura iitwayo 'uundaji wa maneno ambayo inaeleza jinsi ambavyo kiingereza huunda maneno. Wameshughulikia makundi matatu muhimu ambayo ni utumiaji wa viambisho (affixation) kuunganisha maneno (compounding) na kubadili neno la kategoria moja hivi kwa linaweza kutumiwa katika kategoria nyingine (conversion). Kwa mfano, katika Kiswahili neno kulima ni kitenzi na pia laweza kutumika kama nomino:

kulima kwao kulitupendeza.

Pia wametaja njia nyingine zisizo muhimu sana kama vile kule kurudia au kurejelea mzizi (reduplication), kukata schemu ya neno (clipping), kule kuchukua maneno mawili na kuyachanganya ili kuunda neno moja (blending), akronimu na utohozi. Ingawa wameshughulikia uundaji wa maneno katika lugha ya Kiingereza kazi hii itatufaa sana kwa sababu baadhi ya taratibu za uundaji wa maneno katika lugha zote mbili zinashabiniana.

Temu (1984) anasema kuwa kuna taratibu nne zinazotumiwa katika kukitajirisha Kiswahili na istilahi. Hizi taratibu ni kule kuunganisha maneno mawili, kuunda maneno kwa kutumia viambisho, ukopaji na ufupishaji wa maneno. Hapa anataja akronimu kama njia mojawapo ya kufupisha maneno. Baada ya kueleza maana ya taratibu hizi na kutoa mifano kadhaa, anaeleza matatizo yanayotokana nazo. Japo kazi hii imejaribu kueleza njia tofauti tofauti za uundaji wa maneno,

haikuzitalii kwa undani. Kwa mfano, anatueleza kuwa nomino huundwa kutokana na vitenzi na kutupa mifano lakini haelezi ni kwa vipi.

Katika makala mengine ya (1972), Temu anazungumzia juu ya uundaji wa meneno kwa kutumia silabi za Kiswahili Anasema kwamba waliojaribu kuunda maneno hapo awali walitumia njia kama vile kuunganisha maneno, kuunda maneno kwa kutumia viambisho, mnyambuliko, ukopaji na tafsiri mikopo. Katika utumiaji wa kompyuta, Temu anachukulia maneno kuwa hayana maana ya kiasili. Maneno hupata maana yakianza kutumiwa. Hivyo basi anayapa maana na kutumia miundo mingi ambayo ilikuwa haitumiki hapo awali. Maneno yanayohitajika ni yale ambayo yanaafikiana na fonolojia na sarufi ya lugha inayoshughulikiwa (Kiswahili). Temu anaonyesha kuwa ni asilimia ndogo sana ya maneno yanayoweza kutumiwa ambayo hutumika. Kitakachotusaidia kutokana na kazi hii ni orodha ya maneno aliyoyatoa.

Mutahi (1986) anaeleza historia ya upanuzi wa lugha ya Kiswahili na asasi zilizohusika nchini Kenya na vile vile Tanzania. Anaendelea kusema kuwa upanuzi wa istilahi hutokana na njia mbili muhimu; ukopaji na uundaji wa maneno. Maneno hukopwa kutokana na lugha nyingine za Kibantu au lugha ngeni. Pia anataja njia ambazo kwazo maneno yaliyoundwa yalienezwa. Kwa

mfano, katika redio, magazeti, vijitabu, majarida na kadhalika. Kazi hii imejikita zaidi upande wa historia ya upanuzi wa lugha na hivyo basi haikuingilia swala la njia mbalimbali za uundaji wa nomino kwa undani.

Kazi nyingine muhimu kwetu ni ile ya Mdee (1986). Kuhusu uundaji wa istilahi na matatizo yanayotokea, anasema:

> "Kinyume na uundaji wa maneno katika lugha ya kawaida, istilahi aghalabu huundwa na mtu mmoja au watu wachache kwa ajili ya watu wengine. Kwa hali hii, mara nyingine baadhi ya istilahi zilipingwa na watumiaji kwa sababu hawakuelewa misingi iliyotumiwa katika uundaji wake au hawakupenda istilahi kwa sababu hazioani na dhana zinazowakilisha au kwa sababu wengine hupenda istilahi fulani kwa sababu ya upya au shani yake na bado wengine watazipenda istilahi za aina fulani kwa ajili ya mazoea tu" 2

Anaeleza njia kadhaa za uundaji wa istilahi kama vile uundaji wa istilahi wa nasibu, uhusiano baina ya dhana na kitajwa, utohoaji, ufupishaji wa istilahi kikundi na kutafsiri istilahi zilizo katika lugha za kigeni. Japo hatutashughulikia uundaji wa istilahi kwa undani, kazi hii itatufaa sana kwani baadhi ya njia anazoeleza za kuundia istilahi pia zaweza kutumika na nyingine tayari hutumika kuundia nomino za kawaida.

Katika kitabu chake kilichochapishwa mwaka huo huo wa 1986, katika sura iitwayo 'uundaji wa msamiati mpya kwa uambishaji ' Mdee anatangulize kwa kusema kuwa baadhi ya mbinu za uundaji msamiati mpya ambazo hutumiwa na waundaji wa maneno ni pamoja na kunyambua na kuambisha maneno kwa vipande vya maneno viitwavyo viambishi, kukopa na kutohoa, maneno ya lugha nyingine, kufupisha maneno marefu kwa kuunga silabi za mwanzo na kuunganisha maneno mawili au zaidi ili kupata neno moja.

Anaorodhesha mambo muhimu katika kuunda neno jipya kuwa ni kuainisha dhana, kuainisha maneno yenye maana ya msingi na kuteua viambishi vijenzi. Dosari moja katika kazi hii ni kwamba Mdee anachukulia maneno kama vile <u>tega</u>, <u>cheza</u>, <u>fungua</u>, <u>kinga</u>, <u>piga</u>, n.k. kuwa ni mizizi. Lakini mizizi ya maneno haya ni -teg-, -chez-, -fung-, -king-, -pig- n.k. Vile vile anatoa mifano ya maneno yanayoundwa kwa kutumia viambisho {ki}, {m-}, {n}, {ji}, {u} na {i}.

Akida (1983) anatoa sababu za kukuza msamiati wa Kiswahili. Anasema kuna njia tatu muhimu na rahisi za kuunda msamiati nazo ni njia isiyo rasmi, njia rasmi na njia ya kuunda na kutunga maneno mapya. Njia isiyo rasmi ni ile ya kukusanya maneno mapya kutoka magazetini,

redioni, katika baraza za mahakimu, vyuo kama vile vya tiba, uhandisi, kutoka viwandani, madukani, kwenye televisheni na kadhalika. Njia rasmi ni kule kupata msamiati kutoka katika vyombo halisi ambavyo ndivyo vinavyotumainiwa kutoa msamiati unaokubalika kwa mfano BAKITA (Baraza la Kiswahili la Taifa) au TUKI (Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili). Katika njia za kuunda na kutunga maneno mapya, ana makundi matatu ambayo ni uundaji wa kiwastani, uundaji wa kiuzoefu na uundaji wa kimataifa. Kwa muhtasari, ametaja mambo kama vile kupata tafsiri ya moja kwa moja, kule kupata tafsiri kwa kuhusisha kitu chenyewe na umbo lake, kazi yake au kwa kutafuta maelezo. Pia ametaja utohozi. Ingawa kazi hii inahusu mada yetu, imejikita zaidi upande wa matatizo yanayomkabili muundaji wa istilahi.

Gibbe (1983) anaanza makala yake kwa kueleza faida ya istilahi. Kuhusu uzalishaji wa istilahi za Kiswahili anataja njia mbalimbali kama vile maneno - pacha, maneno ya kigeni, utohozi, maneno kutokana na lugha za Kibantu, uchambuzi wa sarufi ya Kiswahili na matumizi ya kompyuta.

Swala la msamiati wa kisayansi limeshughulikiwa sana na wasomi kadha wa kadha. Akida amekitokeza na msamiati wa muda wa sayansi (Elimuviumbe) katika majarida kadha

wa kadha kama vile Kiswahili Vol 45/1, 43/2, 41/1 na 2 Anachokifanya Akida ni kutaja neno kwa kiingereza, kulipa tafsiri ya Kiswahili na vile vile kuonyesha jinsi tafsiri hiyo ilivyopatikana. Archbold (1973) pia anashughulikia msamiati wa Elumuviumbe ambapo anatoa msamiati, anaeleza maana yake na kutoa tafsiri yale ya Kiingereza.

Gurnah (1974) katika makala yake kuhusu elimu mapando, anataja neno, kisha anatoa tafsiri yake na kusema jinsi lilivyoundwa. Kwa mfano ikiwa liliundwa kutokana na fasihi ya kilimo katika Kiswahili au linatumiwa mno katika matumizi ya kawaida na wakulima wa Kenya na Tanzania. Vile vile lawezakuwa limetafsiriwa moja kwa moja kutoka Kiingereza au kuchukua neno linalo-karibiana sana na dhana inayotakiwa na kulipa maana mpya. Pia anasema ikiwa neno linatokana na kufupishwa kwa maneno mawili au matatu ya Kiswahili. Maneno mengine yanatokana na uundaji wa moja kwa moja au kutumia maneno yanayotumika katika lugha nyingine za Kibantu. Pia anataja kuwa maneno mengine yanatokana na Kiingereza Kiarabu na Kihindi hasa Kigujerati.

Msamiati mwingine uliosshughulikiwa ni msamiati wa muda wa hesabu (Vol 45/2), msamiati wa muda wa Chuo Cha Tanu Kivukoni (Vol44/1), msamiati wa muda wa Saikolojia (44/2), msamiati wa kanisa Katoliki (vol.43/2 na kadhalika.

Umuhimu wa kazi hizi zote ni kuwa maneno yaliyoorodheshwa yatatufaa sana. Yatatusaidia kutambua ni njia zipi zilizotumika katika kuyapata.

Kiingi mwaka wa (1982), (1984) na (1987) pia amejishughulisha na msamiati wa kisayansi na kueleza baadhi ya matatizo yanayokikabili Kiswahili katika ukuzaji wa msamiati wa kisayansi. Anasema kuwa Kiswahili hakiwezi kuendelea bila maneno ya kukopa. Anaendelea kudai kuwa hakuna yeyote anayeweza kusema kuwa Kiswahili chaweza kubuni msamiati wake pekee wa maneno ya kisayansi na kitekinolojia.

Mkelle (1971) anazungumza kuhusu maneno ya mkopo yaliyobadilika maana au matumizi yake kufifia baada ya kuingia katika lugha pokezi na sababu za kutokea hivi.

Mbaabu (1985) ameshughulikia ngeli na wiano katika sentensi kwa kutegemea ngeli iliyotumiwa. Amegusia uundaji wa nomino na kutaja njia kadha wa kadha zinazotumiwa kwa mfano mnyambuliko, kuunganisha maneno, na uundaji wa maneno kwa kutumia kiambisho cha ngeli ya 15 yaani {ku}. Pia amezungumzia juu ya uundaji wa nomino kwa kutumia viambisho vifuatilizi {i}, {e}, {o}, {u} na {a} kutokana na maneno yaliyoazimwa.

Kazi hii haitofautishi vilivyo njia mbalimbali za uundaji wa nomino kwa mfano baina ya uambishaji na unyambuaji. Vile vile kazi hii ina dosari nyingi sana

kwa mfano Mbaabu anasema kuwa:

> 'majina kama vile mpiga pigo, na mlo yameundwa kutokana na vitendo ambavyo havijafanyiwa mabadiliko yoyote'3

Tunajua kuwa nomino hizi zimeundwa kutokana na mizizi ya vitenzi pamoja na viambisho vitangulizi vya ngeli na viambisho vifuatilizi ambavyo ni mofimu maalum za kubadilisha vitenzi kuwa nomino.

Kapinga (1983) katika sura iitwayo 'Mnyambuliko' anasema kuwa kunyumbua ni kurefusha kitu kama mpira. Anaendelea kusema kuwa mnyambuliko ni hali ile ya kulipa neno maana nyingine kwa kuongezea viambisho fulani fulani. Kulingana na mifano anayotoa, Kapinga hatofautishi baina ya unyambuaji na uambishaji.

Anasema kuwa katika kuunda nomino viambisho vinavyohusika ni viambisho awali na viambisho tamati. Viambisho awali huwa kwa kawaida ni viambishi - ngeli. Navyo viambisho tamati vinavyotumiwa ni {i}, {ɨi}, {e}, {o}, {fu/vu}, na {a}. Kinyume na dai la Kapinga kuwa {a} hutumiwa kuunda nomino, sisi tunaamini kwamba {a} haitumiki kuunda nomino kutokana na mizizi ya asili ya Kibantu. {a} hutumiwa tu kuunda nomino kutokana na mizizi iliyoazimwa kutoka lugha nyingine. Kapinga anataja kwa kupita njia nyingine zinazotumiwa kuunda

nomino kama vile kuunganisha maneno, kutohoa maneno ya mikopo na kunyambua vitenzi vilivyokopwa.

Katika makala yake ya 1975, Kapinga amegusia uundaji wa nomino lakini ameelemea zaidi upande wa Mnyambuliko wa maneno. Kama katika kazi yake ya (1983) ambayo tumeiangalia hapo juu, Kapinga hatofautishi baina ya uambishaji na unyambuaji. Vile vile kwa sababu ya kushughulikia vipengee kadha vya lugha kwa pamoja kazi yake inakanganya msomaji.

Kazi nyingine ambazo zimefanywa kuhuzu mada hii ni kama vile makala yaliyoandikwa na Mbunda (1976). Katika kazi hii Mbunda amejaribu kueleza nomino ni nini na jinsi zinavyopangwa katika makundi. Kwa njia nyingine ameshughulikia zaidi upande wa ngeli za Kiswahili.

Naye Besha (197 7) katika jarida la <u>Mulika</u> 3 pia amegusia nomino za Kiswahili. Kazi hii inazungumza juu ya namna ya kupanga maneno ya Kiswahili katika makundi na jinsi mtu anavyoweza kutambua neno fulani liko katika kundi gani. Anasema kuwa upangaji wowote wa maneno ni lazima uonyeshe sababu za kuyapanga hivyo, sababu ambazo zitapatikana katika kuchunguza sarufi nzima ya lugha na wala sio kwa kutazama neno moja. Kazi hii pia imejikita zaidi upande wa ngeli na wiano

wa sentensi nzima kutegemea nomino iliyotumiwa. Kando na kuwa haina chochote cha kutufaa katika utafiti wetu, kazi yenyewe ilikusudiwa kuwa ya kiwango cha shule za sekondari na kwa sababu hii haina uzito wa kutosha.

## 1.5 UPEO WA TASNIFU

Kuna tofauti ndogo sana baina ya msamiati na istilahi. Msamiati ni neno la kijumla la maneno yanayounda lugha ilhali istilahi hutumika kwa maana finyu zaidi kumaanisha maneno ya kitaalamu. Katika tasnifu hii tutashughulikia msamiati wa kawaida. Hata hivyo, tutataja istilahi ambazo hutumika kama msamiati wa kila siku. Pia ni muhimu kutaja hapa kuwa njia mbalimbali ambazo hutumiwa kuunda istilahi vile vile hutumiwa kuunda msamiati wa kawaida. Lakini mifano tutakayotoa itatokana na msamiati wa kawaida.

Tasnifu hii haitashughulikia uundaji wa kategoria nyingine za maneno. Pia haitaingilia sana upande wa ngeli isipokuwa pale ambapo inahitajika ili kuweka utaratibu fulani wazi zaidi.

Fonolojia ya lugha itashughulikiwa pale tu ambapo itakuwa muhimu kuonyesha kwa nini neno fulani linabadilika. Kando na hivi haitaingilia suala la

fonolojia ya Kiswahili kwa undani.

## 1.6 MSINGI WA NADHARIA

Madhumuni ya nadharia ni kuzipa mwelekeo fikira za kitaalamu. Wanaisimu na wasomi wamezingatia taratibu mbalimbali katika uundaji wa msamiati.

Baadhi ya wanaisimu na wasomi wameshughulikia uundaji wa maneno kwa kutumia mizizi asilia ya Kiswahili. Mifano ya wataalamu hao ni Polome (1967), Mbaabu (1985), Myachina (1981) Trager (1973) n.k.

Kundi lingine ni lile la wasomi ambao wanatizama uundaji wa maneno kutokana na mizizi au maneno yaliyokopwa. Kwa mfano Zawawi (1979), Krumm (1940), Mdee (1986) n.k.

Hata hivyo, katika utumiaji wa utaratibu wowote ule ni sharti sarufi ya lugha inayohusika (Kiswahili) izingatiwe. Kama wanavyosema Quirk, Greenbaum, Leech na Svartvik (1972), Sheria za uundaji wa maneno ni muhimu sana katika somo la safuri kwa sababu mbili. Kwanza, Sheria hizi hutusaidia kutambua kategoria ya neno fulani kwa kuangalia muundo wake. Pili, zinatufunza kuwa kuna hali ya unyumbufu katika utumiaji wa sheria za sarufi hivi kwamba, mwenyeji wa lugha fulani

anaweza kuhamisha maneno kwa kuongeza au kutoongeza viambisho au maneno mengine, kutoka kategoria moja hadi nyingine.

Tumeyazingatia maoni ya wanaisimu hawa kwa sababu katika Kiswahili, nomino huundwa kwa kutumia njia mbili muhimu. Kwanza, nomino huundwa kutokana na mizizi ambayo tayari iko katika Kiswahili kwa kufuatia sheria za sarufi. Pili, hundwa kutokana na maneno au mizizi iliyokopwa kutoka lugha nyingine. Mikopo hii pia sharti aimbatanishwe na muundo wa Kiswahili ili iafikiane na sarufi ya lugha hii.

Tasnifu hii itatizama aina zote mbili za uundaji wa nomino katika Kiswahili.

## 1.7 NJIA ZA UTAFITI

Kwa kiasi kikubwa utafiti wetu umekuwa wa maktabani. Tumesoma vitabu na makala katika majarida au vijitabu tulivyopata kuhusu mada hii vile vile tumeyasoma makala yoyote tuliyopata ya kitekinolojia yaliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Makala mengi ya kitekinolojia huwa na maneno mapya. Kazi hizi zote zimetupa msingi thabiti wa kuweza kulikabili somo letu kwa njia inayofaa.

Vile vile katika uchunguzi wetu tumesoma magazeti yanayochapishwa kwa lugha ya Kiswahili humu chini. Kwa kuyasoma magazeti haya, tulitarajia kupata nomino mpya ambazo zinatumika katika mawasiliano na kuchunguza jinsi zilivyoundwa. Katika tasnifu hii tumechukulia 'nomino mpya' kama nomino ambayo haipatikani katika kamusi yoyote ya Kiswahili.

Pia tumesikiza taarifa za Kiswahili kwenye redio na televisheni. Vituo tulivyosikiliza ni kama idhaa ya Kiswahili ya sauti ya Kenya, Ujerumani Magharibi, Uingereza na idhaa ya sauti ya Tanzania. Tulipokuwa tunasikiza, tuliandika nomino zozote zilizokuwa mpya kwetu na kuchunguza jinsi zilivyoundwa.

Tumejaribu kuchunguza jinsi ambavyo wazungumzaji wa kawaida wa Kiswahili wanavyounda nomino mpya ili kukabiliana na tajriba mpya katika maisha yao ya kila siku. Tumefanya hivi kwa kuwahoji watu na pia kwa kusikiliza mazungumzo ya makundi ya watu.

Mwisho, tumewahoji wataalamu na wasomi wengine wa lugha hii na kuyachambua maoni yao kuhusu mada hii.

# TANBIHI

1. Tumelitumia neno hili kwa maana ya kule kulibana swala fulani hivi kwamba halina nafasi ya kutosha kujieleza au kuelezwa kwa kikamilifu.

2. Mdee J.S. (1986) "Matatizo ya kuunda istilahi kama yanavyojitokeza katika Kiswahili" Katika jarida la Kiswahili Vol 52/1 na 2 Uk.. 116.

3. Mbaabu, I (1985) Sarufi ya Kiswahili: Nairobi Kenya Publishing and Book Marketing Co. Ltd. UK. 107.

# SURA YA PILI

## 2.0 UTANGULIZI

Katika sura hii tutaangalia fonolojia na mofolojia ya Kiswahili kwa muhtasari. Kisha tutaangalia taratibu za unyambuaji na uambishaji na vile vile dhana nyingine zinazohusiana nazo. Hii ni sura inayoshughulikia uundaji wa nomino kwa kutumia mizizi asilia ya Kiswahili (yenye asili ya kibantu).

## 2.1 FONOLOJIA YA KISWAHILI

Katika sehemu hii mambo tutakayoshughulikia ni yale yanayohusiana moja kwa moja na uundaji wa nomino.

### 2.1.1 VOKALI

Kiswahili kina vokali tano ambazo ni /i/, /u/, /e/, /o/ na /a/. Sifa za vokali hizi huelezwa kwa kuzingatia jinsi zilivyotamkwa: Sehemu ya ulimi inayohusika (mbele, katikati au nyuma) na kiwango ambacho ulimi umeinuliwa (ikiwa umeinuliwa kabisa, wastani au umelalia sakafu ya kinywa). Mpangilio wa vokali katika Kiswahili uko hivi:-

| | Mbele | | nyuma |
|---|---|---|---|
| juu | i | | u |
| katikati | ɛ | | ɔ |
| chini | | a | |

Vokali za mbele huathiriwa na mabadiliko ya aina moja na vile vile za nyuma huathiriwa na mabadiliko ya aina yake. Baadhi ya vokali hizi hubadilika zikitangulia au kufuatwa na vokali fulani. Mabadiliko yanayozikumba vokali ni kama vile:-

2.1.1.1. (a) KUPATA NUSU VOKALI

Nusu vokali ambazo hupatikana ni /j/ na /w/.

Vokali /u/ hubadilika na kuwa nusu vokali /w/ katika mazingira ya kufuatwa na vokali yoyote ile isipokuwa /u/.

SHERIA "A"

/u/ → w/ – [i, a, e, ɔ] Kwa mfano /mu+ana/ → [mwana]

/mu+embe/ → [mwembe]

Nayo vokali /i/ hubadilika na kuwa nusu vokali /j/ ikiwa imeitangulia vokali nyingine yoyote ile isipokuwa /i/.

SHERIA "B"

/i/ → [j] - {e, a, ɔ, u} kwa mfano / vi + ombo/ → [vyombo]

[+juu, +mbele] → j

.1.1.2 (b) KUUNGANA KWA VOKALI MBILI KUWA MOJA

mifano

| | |
|---|---|
| /a/+/i/ → /ɛ/ | /ma + iŋgi/ → [meŋgi] |
| /a/+/ɔ/ → /ɔ/ | /wa+ote/ → [wote] |
| /a/+/a/ → /a/ | /wa+ana/ → [wana] |
| /a/+/ɛ/ → /ɛ/ | /wa+ema/ → [wema] |
| /a/+/u/ → /u/ | |

Mabadiliko haya hayatokei kila wakati. Kwa mfano tuna maneno kama vile maudhui, kauli na kadhalika ambayo hayabadiliki hata ingawa /a/ inafuatwa na /u/ .

## 2.1.2. KONSONANTI.

Mambo manne muhimu katika utamkaji wa sauti za konsonanti ni kujua mahali pa kutamkia, namna ya kutamkia, hali ya kanda za sauti na mkondo wa kupitia hewa (ikiwa ni kinywani au puani). Mpangilio wa konsonanti za Kiswahili uko hivi:

| | Midomo | mdomo na meno | katikati ya meno | tuta la meno | katikati ya tuta la meno na kaakaa la mbele | kaakaa la mbele | kaakaa la nyuma | koromeo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mtuo-mkwaruzo | | | | | tʃ | | | |
| mtuo | p<br>b | | | t<br>d | | ɟ | k<br>g | |
| mkwaruzo | | f<br>v | θ<br>ð | s<br>z | | ʃ | x<br>ɣ | h |
| Nasali | m | | | n | | ɲ | ŋ | |
| Likwidi | | | | r,l | | | | |
| Nusu-Vokali | | | | | | j | w | |

Vitamkwa huathiriana kwa njia mbili;mahali pa kutamkia na namna ya kutamkia

Mabadiliko yanayozikumba konsonanti za Kiswahili kwa kuzingatia namna ya kutamkia ni kama vile:-

2.1.2.1 BADILIKO LA LIKWIDI KUWA KONSONANTI YA MTUO

SHERIA "C"

(a) r → d/n - mfano /n+refu/ → [ndefu]

(b) l → d/n - mfano /n+limi/ → [ndimi]

kulingana na sheria hii, /l/ na /r/ hubadilika na kuwa /d/ katika mazingira ambayo zinafuata /n/. Hii hutokea ili kurahisisha matamshi.

2.1.2.2 MABADILIKO YANAYOSABABISHWA NA ATHARI YA /i/

Katika Kiswahili sanifu konsonanti za mtuo /p/, /t/, /k/, /b/, /d/ na /g/ huathiriwa na mazingira ya /i/. Hii huzibadilisha konsonanti hizi za mtuo na kuzifanya za mkwaruzo. Sheria zinzotumika hapa ni:-

SHERIA "D"

(i) p → f/-i

mfano: {lap} → /mlapi/ → [mlafi]

(ii) $b \rightarrow \begin{Bmatrix} z \\ v \end{Bmatrix} /-i$

mfano: $\{ib\} \rightarrow$ /muibi/ $\rightarrow \begin{bmatrix} mwizi \\ mwivi \end{bmatrix}$

(iii) $t \rightarrow s/-i$

mfano: {fuat} → /mfuati/ → [mfuasi]

(iv) $d \rightarrow z/-i$

mfano: {pend} → /mpendi/ → [mpenzi]

(v) $k \rightarrow \int /-i$

mfano: {pik} → /mpiki/ → [mpi∫i]

(vi) $g \rightarrow z/-i$

mfano: {jeŋg} → /mjeŋgi/ → [mjenzi]

(vii) $w \rightarrow v/-i$

mfano: {lew} → /mlewi/ → [mlevi]

Hata hivyo kuna maneno mengine ambayo hayabadilishwi na mazingira ya /i/. Kwa mfano neno pindi kutokana na mzizi {pind}, neno mkopi kutokana na mzizi {kop} na kadhalika.

Baadhi ya mabadiliko haya yanayosababishwa na athari ya /i/ ni ya namna na mahali pa kutamkia. Niliyoyataja katika sehemu hii yanazingatia namna ya kutamkia lakini baadhi ya konsonanti zimebadilika pahala pa kutamkia, kwa mfano: $k \rightarrow \int / - i$

Sauti iliyokuwa ikitamkiwa katika kaakaa la nyuma sasa inatamkiwa katika kaakaa la mbele

$p \rightarrow f/ - i$

Sauti iliyokuwa ikitamkwa kwa kutumia midomo miwili inatamkwa kwa kutumia mdomo na meno.

g → Z/-i

Sauti ya kaakaa la nyuma inabadilika na kutamkiwa kwenye tuta la meno.

Imedaiwa kuwa sauti ya likwidi /l/ hubadilishwa na mazingira ya /i/ kuwa /z/ kwa mfano neno mlezi kutokana na kutenzi lea. Nayo nusu-vokali /w/ hubadilika katika mazingira ya /i/ na kuwa /v/ kwa mfano neno mlevi kutokana na kitenzi lewa. Polome(1967). Ukweli wa dai hili hatutauchunguza kwa sababu hauhusu mada yetu.

2.1.2.3. UKAAKAISHAJI

Sheria nyingine katika Kiswahili sanifu inayohusu konsonanti ni ile inayobadilisha /ki/ kuwa /tʃ/ katika mazingira ya kutangulia vokali

SHERIA "E"

Ki → tʃ /-V

mifano /kiumba/ → [tʃumba]

/kiombo/ → [tʃombo]

Sheria yenyewe inamaanisha kuwa sauti ambayo kwa kawaida huwa si ya kaakaa la mbele inabadilika na kuwa ya kaakaa la mbele. Kwa sababu ya mazingira ya kutangulia vokali, /ki/ inabadilika na kuwa /tʃ/

sauti ya mtuo - mkwaruzo inayotamkiwa kwenye kaakaa la mbele.

Sheria hii haitumiki pale ambapo maneno yatagongana na kutatiza mawasiliano. Kwa mfano, kioo halibadiliki kwa sababu litakuwa Choo na kuna Choo nyingine katika Kiswahili. Vile vile neno kiama halibadiliki kwa sababu litakuwa chama na tayari kuna neno chama katika Kiswahili. Bakari (1982) anasema kuwa Sheria hii pia inapatikana katika baadhi ya majina ya ngeli ya tisa ambayo yana {n} kama kiambisho kitangulizi. Sheria hii ndiyo inayoeleza mabadiliko kutoka n - ny - ɲ . Anasema kuwa hapo awali {n} ilikuwa na vokali, yaani ilikuwa {ni} na ndiyo sababu sheria hii ya ukaakaishaji ikapata uwezo au nafasi ya kutumika. Anatoa mifano kama vile;

/ni + umba/→/ny + umba/→ [ɲumba]
/ni + uŋgu/→ /ny + uŋgu/→ [ɲuŋgu]
/ni + asi/→ /ny + asi/→ [ɲasi]
/ni + eusi/→ /ny + eusi/→ [ɲeusi]
/ni + oŋgo/→ /ny + oŋgo/→ [ɲoŋgo]

Katika baadhi ya mifano hii, sheria mbili zimetumika Sheria ya wiano wa nasali na konsonanti inayofuata na sheria ya ukaakaishaji. Kwa mfano [ɲuŋgu] na [ɲoŋgo].

## 2.1.2.4. WIANO WA NASALI NA KONSONANTI INAYOFUATA

Mabadiliko yanayozikumba konsonanti za Kiswahili kwa kizingatia mahali pa kutamkia ni kama vile wiano wa nasali na konsonanti inayofuata. Kwa jumla sheria inayotumika hapa ni

SHERIA "F"

$/Nasali/ \rightarrow [\alpha m] / - [\alpha m]$

Hii ina maana kuwa sauti ya nasali huwiana na pahala pa kutamkiwa konsonanti inayofuata. {n} hubadilika-badilika kutegemea mazingira. Mabadiliko haya ni

SHERIA "G"

(i) $n \rightarrow m / - [b]$

/n/ hubadilika kuwa /m/ katika mazingira ya kufuatwa na sauti ya midomoni. Kwa mfano: /n + boga/ → [mboga]

(ii) $n \rightarrow ɱ / - v$

/n/ hubandilika kuwa /ɱ/ katika mazingira ya kufuatwa na sauti ya mdomo na meno

mfano: /n+vi/ - (ɱvi)

(iii) $n \rightarrow ɲ / - \{ɟ, i\}$

/n/ hubadilika kuwa /ɲ/ katika mazingira ya kufuatwa na sauti ya kaakaa la mbele

mfano: /n+ɟia/ — [ɲɟia]

(iv) n → ŋ /-g

/n/ hubadilika kuwa /ŋ/ katika mazingira ya kufuatwa na sauti ya kaakaa la nyuma

mfano: /n+gumu/ → [ŋgumu]

## 2.1.2.5 KUFUTILIWA MBALI KWA KONSONANTI

Mabadiliko mengine ni yale ya kufutiliwa mbali kwa konsonanti. /r/, /l/ na /g/ hupotea katika Kiswahili. Kutokana na mpangilio unaopendekezwa na Kiswahili, yaani ule wa konsonanti vokali konsonanti vokali (kvkv) inasemekana kuwa maneno mengine kama vile kung'aa na kuzuba yalikuwa na /r/ au /l/ lakini sauti hizi zikapotea kwa sababu za kihistoria. Yasemekana kuwa hapo awali maneno haya yalikuwa kung'ara na kuzubala. Huenda ikawa kauli hii ni sawa kwani hadi leo kunao watu wanaoyatamka yakiwa na /r/ au /l/ badala ya kusema kung'aa au kuzubaa.

Konsonanti nyingine ambayo hupotea katika Kiswahili sanifu ni /g/. Kupotea huku kunatokana na sheria inayoitwa 'Ganda Law'. Sheria hii inasema kuwa konsonanti hupotea pale ambapo inatanguliwa na nasali na kufuatwa na vokali na nasali nyingine.

SHERIA "H"

K → Ø/n - vn.

Kwa mfano katika neno ng'ombe, /g/ inapotea kwa sababu ya kutanguliwa na nasali /n/ na kufuatwa na vokali /O/ na

nasali nyingine /m/. Maneno mengine ambayo yamebadilishwa na sheria hii ni kama vile ng'amua, ng'ang'ana n.k. Hata hivyo, sheria hii pia hutumika pale ambapo /g/ inafuatwa na vokali na konsonanti nyingine ambayo si nasali. Kwa mfano katika neno /ŋara/

## 2.1.2.6. KUONGEZWA KWA KONSONANTI

Badiliko jingine ni lile la kuongezwa kwa konsonanti. Konsonanti hutiwa pale ambapo pana mfululizo wa vokali ili kurahisisha matamshi. Kwa mfano tukiliangalia neno kuteua tungetarajia kupata nomino m-teu-e kutokana nalo lakini tunapata nomino mteule. Pia kutokana na mzizi {nunu} tungetarajia kupata neno nunu-i-a lakini tunapata neno nunulia. Vile vile tunapata neno mnunuzi badala ya mnunu-i, mtembezi badala ya mtembe-i n.k. /l/ na /z/ huongezwa pale ambapo pana mfululizo wa vokali ili kuwa na ule mpangilio wa kvkv na hivyo basi kurahisisha matamshi.

## 2.2 MOFOLOJIA

Mofolojia ni tawi la isimu linaloshughulikia viungo vidogo kabisa katika lugha vyenye maana na mpangilio wa hivi viungo katika kuunda maneno. Kamusi ya istilahi ya Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili (1987) inafafanua mofolojia kama:

> "tawi la isimu ambalo huchunguza maneno na aina za maneono."[1]

Mofimu ni kiungo kidogo kabisa katika lugha chenye maana na ambacho hakikatiki tena upya. Kuna makundi mawili ya mofimu:- (1) mzizi (ii) viambisho. Mzizi ndiyo sehemu inayobeba maana ilhali kiambisho ni mofimu ambayo huunganishwa na mzizi wa neno ili kufafanua au kubadili maana ya neno. Kwa jumla, viambisho ni vya namna tatu.

1) viambisho awali/tangulizi

2) viambisho kati

3) viambisho tamati/fuatilizi

Viambisho tutakavyojihusishanavyo ni viambisho vitangulizi vya ngeli na viambisho vifuatilizi ambavyo hutumiwa kuundia nominc.

Sura mbalimbali za mofimu huitwa alomofu.

Kiswahili sanifu kina ngeli kumi na sita kama ifuatavyo:

| Ngeli | UMBO LA NDANI | UMBO LA NJE |
|---|---|---|
| 1. | mu | [mu] [m̩] [mw] ɸ |
| 2. | wa | [wa] |
| 3. | mu | [mu] [m̩] [mw] ɸ |
| 4. | mi | [mi] [mj] |
| 5. | ɟi | [ɟi][ɗ] |
| 6. | ma | [ma] [m] |
| 7. | ki | [ki] [tʃ] |
| 8. | vi | [vi] [vj] |
| 9. | N | [n] [m] [ɲ][ŋ][ɱ][ŋ̩] |
| 10. | N | " " " " " " |
| 11. | u | [u] [w] |
| 14. | u | [u] [w] |
| 15. | ku | [ku] [kw] |
| 16. | pa | [pa] |
| 17. | ku | [ku] [kw] |
| 18. | mu | [mu] [m̩] [mw] |

## 2.2.1 MABADILIKO KATIKA NGELI YA 1, 3 NA 18

Katika lugha sauti huathiriana ikiwa zinaambatana. Hii husababisha mabadiliko mbalimbali ya kifonolójia. Katika Kiswahili ngeli ya kwanza, ya tatu na kumi na nane huwa na mu kama muundo wa ndani lakini katika umbo la nje, hujitokeza tofauti kutegemea mazingira ambapo mofimu hiyo inajikuta. Kwa kawaida kukitokea mazingira ambapo kuna vokali mbili ambazo ni sawa, kuna tabia ya kuzifupisha kuwa moja. Umbo la nje la kiambisho kitangulizi cha ngeli ya 1,3 na 18 linaelezwa na sheria zifuatazo:-

(i) u → [w] / — {a e o i}

mfano: / mu + ana / → [mwana]

SHERIA "I"

(ii) u → ø / m— [konsonanti]

sauti /u/ hupotea ikiwa imetanguliwa na /m/ na kufuatwa na kosonanti yoyote ile;

mfano; /mu + zuri/ → [mzuri]

/mu + fupi/ → [mfupi]

/mu + kubwa/ → [mkubwa]

(iii) SHERIA "J"

m → [m̩] # — [konsonanti]

mifano: /mu + tu/ → [m̩tu]

/mu + ti/ → [m̩ti]

2.2.2 MABADILIKO KATIKA NGELI YA 2

Mofimu ya ngeli ya pili ni {wa} ambayo ina alomofu mbili [wa] na [we]. [we] inaelezwa na sheria isemayo kuwa vokali ya chini ikifuatana na vokali ya juu husababisha kuundwa kwa vokali wastani (ya katikati).

SHERIA "K"

a + i → e

V [-juu, +chini] + V [+juu, -chini, +mbele] → V [-juu, -chini, +mbele]

mifano: /wa + iŋgi/ → weŋgi

Vile vile badiliko hili linaweza kuelezwa na sheria isemayo kuwa, katika Kiswahili, kukiwa na vokali mbili ambazo ni tofauti, vokali iliyoko katika mofimu itabadilika na kuwiana na ile ilioko katika mzizi wa neno lenyewe.

a + e ⟶ e

mfano: /wa + ema/ ⟶ [wema]

2.2.3 MABADILIKO KATIKA NGELI YA 4

Mofimu ya ngeli ya nne ni {mi} ambayo ina alomofu mbili [mj] na [mi] . [mj] inatokana na badiliko la kupata nusu vokali kutokana na vokali mbili ambalo tumeshalizungumzia katika sehemu ya 2.1.1.1.

mfano: /mi + aka/ ⟶ [mjaka]

2.2.4 MABADILIKO KATIKA NGELI YA 5

Maneno mengi ya ngeli ya tano hayana mofimu {ji} Nafasi ya kiambisho kitangulizi huwa kapa {ø} . Mabadiliko yanayoikumba ngeli hii yameelezwa na sheria zifuatazo. Kwa mfano ili kupata kimiliki langu, sheria zifuatazo zinatumika


li - angu

i ⟶ j ljangu

j ⟶ ø [langu]

## 2.2.5 MABADILIKO KATIKA NGELI YA 6

Mofimu ya ngeli ya sita ni {ma} . Mofimu hii ina alomofu mbili [ma] na [mɛ] . [mɛ] inasababishwa na athari ya mvutano wa vokali /a/ na /i/. Tokeo la mvutano huu ni vokali ya wastani /ɛ/




/i/ inaenda chini na /a/ inaenda juu = /ɛ/ ya katikati

Sheria yenyewe imeelezwa katika sehemu ya 2.1.1.2.

## 2.2.6 MABADILIKO KATIKA NGELI YA 7

Mofimu ya ngeli ya saba ni {ki} na ina alomofu mbili ambazo ni [ki] na [tʃ]. Sheria zinazotumika hapa ni

(i) i ⟶ [j] / — {e, a, ɔ, u}

/i/ hubadilika kuwa /j/ katika mazingira ya kufuatwa na vokali ambayo si /i/.

(ii) SHERIA "K"

k ⟶ [tʃ] /— [j]

(iii) j ⟶ ø / tʃ — V

| mfano: | ki - ama | ki - angu |
|---|---|---|
| i → [j] | kjama | kjangu |
| k → tʃ | tʃjama | tʃjangu |
| j — ø | tʃama | tʃangu |

Maneno kama vile <u>kioo</u> na <u>kiatu</u> hayabadiliki ili yasitatize mawasiliano.

## 2.2.7 MABADILIKO KATIKA NGELI YA 8

Mofimu ya ngeli ya nane ni {vi} ambayo ina alomofu [vi] na [vj]. [vj] ianatokana na badiliko la

$$i \longrightarrow [j] \ / \ __ \left\{ \begin{matrix} e \\ a \\ ɔ \\ u \end{matrix} \right\}$$

ambalo tumeshalieleza katika sehemu ya 2.1.1.1 na kuligusia tena katika sehemu ya 2.2.6.

## 2.2.8 MABADILIKO KATIKA NGELI YA 9

Mofimu ya ngeli ya tisa ni {N}. {N} hujitokeza kama [n], [m], [ɱ], [ŋ] na [ɲ]. {N} ni mofimu ya jumla iliyoundwa kuwakilisha ngeli hii kwa sababu hakuna alomofu iliyo na uhuru wa kutokea katika mazingira mbalimbali. Kila alomofu ina mazingira yake maalum.

Nasali hii hukubaliana na mahali pa kutamkiwa konsonanti inayofuata.

$$/ + nasali/ \longrightarrow [\alpha m] \ / \ - [\alpha m]$$

Mabadiliko yanayotokea ni:-

(i) $N \longrightarrow [m] \ / \ - [b]$

(ii) $N \longrightarrow [ɱ] \ / \ - [ɣ]$

(iii) $N \longrightarrow [ɲ] \ / \ - \begin{bmatrix} ɟ \\ i \end{bmatrix}$

(iv) $N \longrightarrow [ŋ] \ / \ - [g]$

(v) n hutokea kabla ya d/r/z

Kwa maelezo zaidi na mifano, tazama sehemu ya 2.1.2.4.

2.2.9 BADILIKO LA u → w

Badiliko la [u] → [w] hutokea katika ngeli zote zenye [u] kwa mfano ngeli ya 1, 3, 18, 11, 14, 15 na 17. Sheria yenyewe kama tulivyoona katika sehemu ya 2.1.1.1 ni

$$u \rightarrow w \ / - \begin{bmatrix} i \\ a \\ e \\ o \end{bmatrix}$$

vile vile katika ngeli ya 1,3, na 18, sheria ifuatayo inatumika:-

$$u \rightarrow \emptyset \ / \ \underset{\text{.}}{m} - k$$

mifano /mu + zuri/ → [m̩zuri]

/mu + refu/ → [m̩refu]

/mu + le/ → [m̩le]

2.3 UNYAMBUAJI (DERIVATION)

2.3.1 DHANA YA UNYAMBUAJI

Kulingana na Istilahi - Kiingereza - Kiswahili (1987), dhana ya unyambuaji imeelezwa kama:-

"tendo la kupachika
vipashio kwenye kiini
ili kujenga maneno"[2]

Ufafanuzi huu ni finyu kwa sababu hautofautishi baina ya unyambuaji na uambishaji. Katika tasnifu hii tumechukulia unyambuaji kuwa aina ya uundaji wa maneno ambapo viambisho huongezwa kwenye msingi au mzizi wa neno fulani ili kuunda neno jipya au lenye dhana tofauti.

Katika utaratibu wa unyambuaji, msingi au mizizi ya kategoria fulani ya maneno hutumiwa kuunda maneno ya kategoria nyingine. Kwa mfano nomino kadha katika Kiswahili huundwa kutokana na misingi ya vivumishi. Kutokana na msingi -baya tunapata nomino ubaya. Msingi wenyewe ni wa kivumishi lakini unatumiwa kuunda neno la kategoria ya nomino. Huku kuvuka kwa mipaka ya kikategoria ndiko hasa kunakotofautisha unyambuaji na uambishaji.

## 2.3.2 NOMINO KUTOKANA NA MIZIZI YA VITENZI (DEVERBATIZATION)

Hii ni aina moja ya unyambuaji. Utaratibu huu hutumia mizizi ya vitenzi kuunda nomino. Kwa mfano kutokana na mzizi wa kitenzi {pig}, tunaweza kuunda nomino kama vile pigo, mapigo, mpigaji n.k. Na kutokana na mzizi {pik} tunapata nomino kama vile mpishi, mapishi, upishi n.k. Hapa mofimu maalum kama vile {o}, {ɛ}, na {i} hutumiwa ili kubadili kitenzi fulani kuwa nomino. Mofimu hizi huja baada ya mzizi - yaani ni viambisho vifuatilizi. Licha ya hivyo kiambisho kitangulizi hutumiwa ili ile nomino iwe katika ngeli fulani.

Baadhi ya wasomi, akiwemo Polome (1967) wanashikilia kuwa nomino nyingi huundwa kutokana na mizizi ya vitenzi kuliko mizizi mingine. Kwao wao, utaratibu huu ndiyo unaotoa mchango mkubwa zaidi katika uundaji wa nomino za Kiswahili.

## 2.4 UTUMIAJI WA VIAMBISHO

"Msingi" ni umbo ambalo sheria za uundaji maneno hutumiwa kwalo. Nomino huundwa kwa kutumia viambisho kwa njia mbili:

(a) Kwa kuongeza kiambisho kitangulizi kwenye msingi wa neno. Hii yaweza kubadilisha au kutoibadilisha kategoria ya neno lenyewe. Kwa mfano, msingi -ti ukiongezwa kiambisho cha ngeli ya nne mi unakuwa miti. Kuongezwa kwa kiambisho kitangulizi hiki hakukubadilisha kategoria ya neno lenyewe.. Lakini tukiongeza kiambisho kitangulizi cha ngeli ya 15 yaani {ku} kwenye msingi -imba, tunaibadilisha kategoria ya neno hili kutoka kitenzi hadi nomino.

(b) Kwa kuongeza kiambisho kifuatilizi kwenye msingi wa neno. Mara nyingi hii husababisha kubadilika kwa kategoria ya neno hilo. Kwa mfano tukiongeza kiambisho kifuatilizi {o} katika mzizi {pig} , tunapata nomino pigo. Hapa tunaona kuwa kategoria ya neno imebadilika kutoka kitenzi na kuwa nomino.

Kila kiambisho kina maana yake maalum na kinapoongezwa kwenye mzizi au msingi wa neno, maana ya kimsingi ya neno hilo huathiriwa. Ni muhimu kutambua vile vile kuwa baadhi ya viambisho vina maana zaidi ya moja. Mdee (1986) anasema kuwa viambisho vinavyounda maneno mengi

zaidi kuliko vingine huitwa viambisho vya msingi. Anataja {mu} , {ki} , {u} , na {ji} kama baadhi ya viambisho vya msingi.

## 2.4.1 UTUMIAJI WA VIAMBISHO VITANGULIZI

Kiambisho kitangulizi kikiongezwa kwenye msingi wa kitenzi, nomino au mara chache kwenye msingi wa kivumishi, kiambisho hiki cha ngeli hulipa neno maana ya jumla inayohusiana na ngeli hiyo (Mychina 1981). Hivyo basi maneno yaliyonyambuliwa kudokeza mtenda jambo ambaye mara nyingi atakuwa binadamu au mnyama huundwa kwa kuonge viambisho vitangulizi vya ngeli ya kwanza na ya pili.

mifano: {und} ⟶ [mwundaji]
{som} ⟶ [msomi]
{sem} ⟶ [msemaji] n.k.

Mbaabu (1985) anasema kuwa vitenzi vyenye asili ya kibantu huishia kwa vokali /a/. Kwa kuzingatia maoni haya tunakubaliana na Mychina (1981) na Polome (1967) wanaposema kuwa njia moja ya kuunda nomino ni kwa kuongez kiambisho cha ngeli katika shina la kitenzi.

mifano: wiwa ⟶ mwiwa
ganga ⟶ mganga
nywa ⟶ kinywa n.k.

Msimamo huu wetu unakanusha madai ya baadhi ya wasomi akiwemo Kapinga (1983) wanaoshikilia kuwa neno

mganga limeundwa kwa kuongeza kiambisho cha ngeli {m-} na kiambisho kifuatilizi a- kwenye mzizi wa Kitenzi {gang}. Vokali a- katika neno mganga inaonyesha hali ya kitenzi. Mbaabu (1985) anaandika;

> "... kuunda majina kutokana na vitendo hivyo vyenye asili ya kibantu kwawezekana kwa kutumia viishio ambavyo ni irabu zingine zote isipokuwa hiyo a- ambayo ni kiishio cha vitendo vyote vyenye asili ya kibantu."

Anachokifafanua ni kwamba vokali a- haitumiwi kuunda nomino kutokana na vitenzi vyenye asili ya Kibantu. Vokali hii hutumiwa kama mofimu ya kuundia nomino pale tu ambapo kitenzi chenyewe kimekopwa kutoka lugha nyingine zisizo za Kibantu.

### 2.4.1.1 KIAMBISHO {u}

Kiambisho kitangulizi cha ngeli ya 14 huchangia sana katika uundaji wa nomino. Kiambisho {u} cha ngeli ya 14 huunda nomino dhahania. Hizi ni nomino ambazo huwakilisha vitu visivyoshikika na ambavyo vinaonekana katika akili tu. Mdee (1986) anasema:

> "udhahania hujitokeza tu katika maneno yaliyonyambulishwa na kuambishwa u-, sio kwa maneno yaanzayo na herufi u- kama vile ubao, uzi, n.k."

Mofimu {u} huongezwa kwenye misingi ya vivumishi, vitenzi na nomino.

mifano:

misingi ya vivumishi

/u + baya/ ⟶ [ubaya]

/u + zuri/ ⟶ [uzuri]

/u + rembo/ ⟶ [urembo]

misingi ya nomino

/u + kahaba/ ⟶ [ukahaba]

/u + toto/ ⟶ [utoto]

/u + jamaa/ ⟶ [ujamaa]

misingi ya vitenzi

/u + som + i/ ⟶ [usomi]

/u + lim + a+ji/ ⟶ [ulimaji]

/u + fug + a + ji/ ⟶ [ufugaji] n.k.

2.4.1.2 KIAMBISHO {ki}

Kiambisho kitangulizi {ki} hutumiwa kuunda nomino zinazodokeza kitu kinachotenda au kufanyia jambo fulani.

mifano:

kinga ⟶ kikingio

nasa sauti ⟶ kinasa sauti

nywa ⟶ kinywa

chunga ⟶ kichungi n.k.

Katika baadhi ya mifano hii, viambisho vifuatilizi ambavyo hutumiwa kubadilisha kitenzi kuwa nomino vimetumika. Kwa mfano {o} na {i} . Mofimu hizi zitafafanuliwa zaidi katika sehemu ya 2.4.2.

## 2.4.2. UTUMIAJI WA VIAMBISHO VIFUATILIZI

Nomino huundwa kutokana na mizizi au misingi ya vitenzi kwa kutumia mofimu maalum.

### 2.4.2.1 MOFIMU {i}

Mofimu {i} huunda nomino zenye maana tofauti kutegemea kiambisho kitangulizi kilichotumiwa.

{i} ikitumiwa pamoja na kiambisho cha ngeli ya kwanza na ya pili (mu- na wa-) huonyesha mtenzi wa tendo linalohusika.

mifano: /m- pik- i/ ⟶ [mpishi]

/m- sem- i/ ⟶ [msemi]

/m- fuat- i/ ⟶ [mfuasi]

/m- lew- i/ ⟶ [mlevi] n.k.

{i} ikitumiwa na kiambisho cha ngeli ya saba na cha ngeli ya na huonyesha njia au ala inayotumiwa kutenda tendo. Vile vile huonyesha mtu anayetenda tendo linalodokezwa na kitenzi.

| | | |
|---|---|---|
| mifano: <u>ongoza</u> | ⟶ | kiongozi |
| <u>nyoa</u> | ⟶ | kinyozi |
| <u>piga</u> | ⟶ | kipigi |
| <u>fungua</u> | ⟶ | kifunguo |
| <u>fagia</u> | ⟶ | kifagio n.k. |

Wasomi wamejitokeza na maelezo tofauti ya nomino zinazoundwa kwa kutumia {i} pamoja na kiambisho cha ngeli ya sita {ma}. Kwa mfano Mdee (1986) anasema

> "Vitenzi vyenye kuchukua kiambishi tamati -i pamoja na viambishi awali ma- au u- hujenga majina yenye kodokeza hali ya tendo"5

Naye Mbaabu (1985) anasema:

> "Baadhi ya majina yaliyoundwa kwa kutumia kiishio i humaanisha vile kitendo kinavyotendwa. Majina hayo huwa katika ngeli ya 6 Kwa kuwa yana kiambisho /ma/. Majina hayo ni ya vitu visivyoweza kuguswa." 6

Hata hivyo, tunaona kuwa baadhi ya nomino hizi huonyesha namna mbali mbali za kufanya jambo. Kwa mfano <u>mapishi</u>. Mapishi ni namna au njia za kupika na kutayarisha chakula (kamusi ya Kiswahili sanifu 1981). Vile vile nomino nyingine ambazo hutumia {i} pamoja na kiambisho cha ngeli {ma} huonyesha ile hali ya utimilifu wa tendo fulani. Polome (1967)

mifano:-

/ma - pik - i/ ⟶ [mapiʃi]

/ma - omb - i/ ⟶ [maombi]

/ma - zik - i/ ⟶ [maziʃi]

/ma-ongoz - i/ ⟶ [Maoŋgozi]

/ma -pend - i/ ⟶ [mapenzi] n.k.

{i} ikitumiwa na kiambisho cha ngeli ya 14 {u} huonyesha hali yenyewe ya kufanya jambo. Nomino ambazo huundwa kwa njia hii ni nomino dhahania. Hii ina maana kuwa ni nomino ambazo huwakilisha vitu visovyoshikika na ambavyo vinaonekana katika akili tu. (Istilahi - Kiingereza - Kiswahili (1987).

mifano: /U - pik - i/ → [upiʃi]

/U - lew - i/ → [ulevi]

/U - ongoz - i/ → [Uoŋgozi]

/U - tum - ish - i/ → [Utumiʃi]

/U - lind - i/ → [Ulinzi] n.k.

## 2.4.2.2. MOFIMU {ji}

{ji} ni moja kati ya mofimu ambazo zimewahi kutiliwa shaka ikiwa kweli hutumika kuundia nomino. Mbaabu (1985) anaichukulia kuwa ni sehemu ya mofimu {i} . Anasema:

> "Wakati mwingine kiishio i hupatikana kimetanguliwa na j. Badala ya i huwa ji"7

Naye Polome' (1967) anashikilia kuwa mofimu yenyewe ni {aji} na ilitokana na {ag} mofimu ya Kibantu.

Mofimu {ji} mwishoni mwa nomino hudokeza dhana ya mazoea ya kutenda au kutendeka kwa jambo fulani.

{ji} ikiongezwa kwenye msingi ulio na kiambisho cha ngeli ya 1 au ya 2 huonyesha ama mtu anayefanya jambo fulani mara kwa mara au kazi ya mtendaji.

mifano: msomaji — mrushaji
mwimbaji — mlimaji
mchezaji — mwindaji
mfugaji — mwuaji

{ji} ikiongezwa kwenye msingi ulio na kiambisho {u} huleta dhana ya udhahania wa tendo la kimazoea. Nomino ambazo huundwa kwa kutumia kiambisho kitangulizi {u} na mofimu {ji} huonyesha kazi ya mtendaji.

mifano: ulimaji — ujengaji
uwindaji — usafirishaji
uchoraji — ufugaji
uombaji — uuaji

Vile vile kuna nomino chache ambazo huundwa kwa kuengeza {ji} katika misingi yenye viambisho vingine vya ngeli. Kwa mfano {ki} na {mu} ya ngeli ya 3.

mifano: nywa ⟶ kinywaji
tambaa ⟶ mtambaaji

Kuhusiana na uundaji wa nomino kwa kutumia mofimu {ji} mbaabu (1985) anatoa dai kuwa ikiwa misingi ya vitenzi inaanza kwa konsonanti ambazo hazina msepetuko wa

kanda za sauti, basi nomino zitakazoundwa zitaishia kwa {ji} .

> "Kitendo kinapoanzia kwa konsonanti isiyo ya kukaza pumzi kama vile <u>tazama</u>, <u>sikia</u> na <u>chunga</u>, majina yanayoundwa huishia kwa ji kama vile <u>mtazamaji</u>, <u>msikilizaji</u> na <u>mchungaji</u>"8

Twnaona vigumu sana kukubaliana na dai la Mbaabu (1985) kwa sababu kuna nomino nyingi sana ambazo zimeundwa kwa kuongeza {ji} kwenye misingi ya vitenzi vinavyoanza kwa konsonanti zenye msepetuko wa sauti. Kwa mfano konsonanti kama vile /b/, /d/, /g/, /l/, /r/, /n/, /h/, n.k.

| | | |
|---|---|---|
| mifano: | m<u>b</u>atizaji | m<u>g</u>awanyaji |
| | m<u>g</u>awaji | m<u>g</u>omaji |
| | m<u>h</u>amiaji | m<u>l</u>umbaji |
| | m<u>l</u>indaji | m<u>n</u>enaji |
| | m<u>l</u>ipaji | m<u>n</u>unuaji |
| | m<u>r</u>ukaji | m<u>r</u>ushaji |
| | m<u>z</u>ungumzaji | m<u>z</u>ururaji |
| | m<u>l</u>imaji | |

Kila sheria sharti iwe na upeo wake. Hata hivyo, ili sheria fulani ikubalike kuwa ni sheria katika lugha fulani, haina budi kutumika katika mingi ya mifano na kuacha kando mifano michache sana. Lakini kuhusiana na suala hili, mifano tulioipata si michache kamwe.

2.4.2.3. MOFIMU "ZI"

Kumekuwa na tashwishi miongoni mwa wataalamu kuhusu utumiaji wa mofimu {zi} kuundia nomino. Wasomi kadha akiwemo Mbaabu (1985) wamesisitiza umuhimu wa kufanya uchunguzi zaidi kuhusu mofimu hii.

Katika sehemu ya 1.2., tulitaja mofimu {zi} kuwa mojawapo ya zile ambazo tungechunguza ikiwa kweli zinatumiwa kuunda nomino. Kuhusu uundaji wa nomino kwa kutumia {zi}, Mbaabu (1985) anasema

> "....ikiwa kitendo huanzia kwa konsonanti ya kukaza pumzi au ikiwa kiini cha kitendo hicho kitaishia kwa konsonanti ya kukaza pumzi, mara nyingi jina linaloundwa litaishia kwa zi."9

Ni maoni yetu kuwa Mbaabu (1985) anatizama suala hili kwa njia dhaifu. Myachina (1981) anaonekana kuwa na mwelekeo sawa zaidi anaposema kuwa {zi} yaweza kuwa sura nyingine ya {ji} na hutumika pale ambapo misingi inamalizikia kwa vokali mbili.

Kutokana na uchunguzi wetu, tunapendekeza kuwa [zi] haitumiki kuunda nomino. [Zi] ambayo inapatikana mwishoni mwa nomino inatokana na taratibu mbili za kifonolojia.

(a) Kila lugha ina muundo wake maalum wa silabi unaopendekezwa. Kiswahili hupendekeza muundo

wa KVKV. Itokeapo kuwa neno lina mfululizo wa vokali, konsonanti huongezwa ili kurahisisha matamshi. Konsonanti ambazo huongezwa ni /z/ na /l/ kama tulivyoona katika sehemu ya 2.1.2.6. Kwa mfano, tuliona kuwa mofimu {i} ikiongezwa kwenye msingi wa kitenzi ulio na kiambisho cha ngeli ya kwanza, nomino inayopatikana inadokeza mtenzi wa tendo fulani.

Chambua → /m-chambu-i/ → [mchambuzi]

katika mfano huu tungetarajia kupata nomino mchambui. Lakin tunapata mchambuzi kwa sababu ya kuongezwa kwa /z/ ili kuvunja mfalulizo wa vokali.

mifano:

nyoa → /ki - nyo - i/ → [kiɲozi]
kaa → /m - ka - i/ → [mkazi]
lea → /m - le - i/ → [mlezi]
zaa → /m - za - i/ → [mzazi]
Chungua → /m - chungu-i/ → [mchuŋguzi]
Okoa → /u - Oko - i/ → [uokozi]

(b) Zi mwishoni mwa nomino vile vile inatokana na athari ya /i/ ambayo hubadilisha konsonanti za mtuo na kuzifanya za mkwaruzo. Tazama sehemu ya 2.1.2.2.
Udhoofishaji

d → z/-i

g → z/ - i

b → {z, v} / - i

Hii inamaanisha kuwa, tukiwa na mzizi au msingi wa kitenzi unaoishia kwa mojawapo ya /d/, /g/ au /b/ na tukiuongeza mofimu {i}, {i} hii itaathiri konsonanti hizi na kuzibadilisha kuwa /z/. Ndiyo maana tunapokuwa na mzizi {pend} na kuuongeza kiambisho cha ngeli ya kwanza {mu} na mofimu {i} ya mtendaji, tunaoata nomino mpenzi na wala sio mpendi.

mifano: jenga → /m - jeng - i/ → [mjenzi]

linda → /m - lind - i/ → [mlinzi]

loga → /m - log -i/ → [mlozi]

iba → /m - ib - i/ → [mwizi] .

Wakati mwingine /z/ huwa ni sehemu ya mzizi. Kwa mfano katika nomino kiongozi ambayo Mbaabu (1985:110) ameitaja kimakosa kama mfano wa nomino zinazoundwa kwa kutumia mofimu {zi} . Nomino hii imeundwa kutokana na kiambisho kitangulizi {ki}, mzizi {ongoz} na mofimu {i} .

2.4.2.4 MOFIMU {ɛ}

Mofimu nyingine inayotumiwa kuunda nomino ni {ɛ}. {ɛ} huunda nomino zinazoonyesha hali ya kutendwa. Nomino hizi huonyesha mtu au kitu ambacho kimetokana na kitendo fulani. Kwa njia nyingine ni hatima au tokeo la kitendo fulani. Nomino ambazo huundwa kwa kutumia mofimu {ɛ} huweza kuchukua viambisho vya

Hii inamaanisha kuwa, tukiwa na mzizi au msingi wa kitenzi unaoishia kwa mojawapo ya /d/, /g/ au /b/ na tukiuongeza mofimu {i} , {i} hii itaathiri konsonanti hizi na kuzibadilisha kuwa /z/. Ndiyo maana tunapokuwa na mzizi {pend} na kuuongeza kiambisho cha ngeli ya kwanza {mu} na mofimu {i} ya mtendaji, tunapata nomino mpenzi na wala sio mpendi.

mifano:
- jenga → /m - jeng - i/ → [mjenzi]
- linda → /m - lind - i/ → [mlinzi]
- loga → /m - log -i/ → [mlozi]
- iba → /m - ib - i/ → [mwizi]

Wakati mwingine /z/ huwa ni sehemu ya mzizi. Kwa mfano katika nomino kiongozi ambayo Mbaabu (1985:110) ameitaja kimakosa kama mfano wa nomino zinazoundwa kwa kutumia mofimu {zi} . Nomino hii imeundwa kutokana na kiambisho kitangulizi {ki}, mzizi {ongoz} na mofimu {i} .

#### 2.4.2.4 MOFIMU {ε}

Mofimu nyingine inayotumiwa kuunda nomino ni {ε}. {ε} huunda nomino zinazoonyesha hali ya kutendwa. Nomino hizi huonyesha mtu au kitu ambacho kimetokana na kitendo fulani. Kwa njia nyingine ni hatima au tokeo la kitendo fulani. Nomino ambazo huundwa kwa kutumia mofimu {ε} huweza kuchukua viambisho vya

ngeli ya 1,2,3,4,7,8,9 na 11.

mifano: <u>teua</u> → mteule/wateule

<u>tuma</u> → mtume/mitume

<u>kata</u> → mkate/mikate

<u>peta</u> → pete

<u>shiba</u> → shibe

<u>shinda</u> → mshinde/wasinde

<u>vimba</u> → uvimbe

<u>pinda</u> → upinde

<u>shinda</u> → ushinde

### 2.4.2.5 <u>MOFIMU {O}</u>

Mofimu {O} huunda nomino ambazo huleta maana mbili:-

(a) Mofimu hii huunda nomino ambazo huonyesha hatima au tokeo la kitendo au jambo fulani

(b) Huunda nomino ambazo huonyesha chombo au ala ya kufanyia jambo fulani.

Mofimu {O} inaweza kutumiwa pamoja na mizizi au misingi ya vitenzi vyenye viambisho vya ngeli ya 3,4,5,6,7,8,9,10 na 11. Mifano ya nomino zinazoonyesha vyombo vya kufanyia tendo fulani ni kama vile:-

| | |
|---|---|
| kifuniko | kifungo |
| kizibo | masikio |
| mtego | ufunguo |
| kipigo | nyundo |

Neno nyundo limetokana na kuongeza mofimu{o} kwenye mzizi wa kitenzi und na kiambisho cha ngeli ya ya tisa {n} . Taratibu za kifonolojia zinazotumika hapa ni zile za upataji wa nusu vokali kutokana na vokali mbili na ukaakaishaji. Taratibu zote mbili tumeshazieleza kwa uwazi katika sehehmu 2.1.1.1 na 2.1.2.3.

Mifano ya nomino zinazoonyesha hatima ya kitendo ni kama ifuatayo:-

| | |
|---|---|
| msemo | tendo |
| mchezo | tegemeo |
| mapambo | mapatano |
| wimbo | ukumbusho |
| mwanzo | ndoto |

Nomino ndoto imetokana na kitenzi ota. Inasemekana kuwa kitenzi hiki kilikuwa na /l/. Yaani kilikuwa lota (Polome 1967). Hii ina maana kuwa neno hili lilikumbwa na badiliko la l → d/n- (Tazama sehemu ya 2.1.2.1). Kauli hii inatiliwa nguvu zaidi na baadhi ya lugha nyingine za Kibantu ambazo zingali zinatumia neno lota kwa maana ya ota. Mfano mmoja ni Kimeru. Kikikuyu nacho hutumia neno rota kwa maana hiyo hiyo ya ota.

Kama tulivyoona awali, /l/ na /r/ hukumbwa na badiliko hili la kuwa /d/ katika mazingira ya kufuata /n/. /l/ na /r/ ni sauti za likwidi ambazo hukumbwa na mabadiliko sawa na kwa hivyo hakuna tofauti ikiwa neno lenyewe ni <u>lota</u> au ni <u>rota</u>.

Kuhusiana na uundaji wa nomino kwa kutumia mofimu {o}, Mdee (1986) anatahadharisha kuwa

> "mtindo huu wa uundaji wa maneno mapya huweza kuunda maneno yasiyo ya kawaida ambayo, japokuwa yanafuata mfumo wa uundaji maneno unaokubalika, mara nyingine huunda maneno yasiyokubaliwa na wazungumzaji wa lugha"[10]

Anatoa mifano kama vile

| | | |
|---|---|---|
| fika | —— | mfiko |
| ja | —— | mjo |
| lima | —— | mlimo |
| kimbia | —— | mkimbio n.k. |

## 2.4.2.6 <u>MOFIMU {fu(vu)}</u>

Mofimu nyingine ambayo hutumiwa kuunda nomino ni {fu(vu)}. Polome (1967) na Mbaabu (1985) wanaiita mofimu {u}. Lakini tunaiita {fu(vu)} kwa sababu hakuna mahali popote ambapo tulipata /u/ bila kuandamana na ama /f/ au /v/. Mofimu hii kwa jumla huonyesha hali fulani. Humaanisha ama hali au mtu aliye katika

hali fulani. Mofimu hii inaweza kutumika pamoja na viambisho vitangulizi vya ngeli ya 1, 2, na 14. Mara nyingine maana ya utimilifu huonyeshwa kwa kutumia kiambisho {ma} .

mifano:

| | |
|---|---|
| ngeli ya 1,2, | mtulivu/watulivu |
| | mtukufu/watukufu |
| | mlegevu/walegevu |
| | mwaminifu/waaminifu |
| ngeli ya 14 | utulivu |
| | utukufu |
| | ulegevu |
| | upungufu |
| | upotevu |
| ngeli ya 6 | maumivu |
| | maonevu n.k. |

Polome (1967) anasema kuwa vitenzi vilivyokopwa kutoka kiarabu huwa na mofimu {ivu(ifu)} badala ya {fu(vu)}. Kwa mfano <u>haribifu</u> kutokana na kitenzi <u>haribu</u>. Kauli hii tumeikubali kwa sababu hatukupata ushahidi ulio kinyume.

Kuhusu matumizi ya ama {fu} au {vu}, tumegundua kuwa isipokuwa katika maneno machache sana, {vu} hutumika pale ambapo kitenzi kinaishia kwa vokali mbili na {fu} pale ambapo herufi mbili za mwisho ni konsonanti na vokali. Maneno tuliyopata ambayo hayakubaliani na utaratibu huu ni kama vile <u>upungufu</u>, <u>ustarehevu</u> na <u>utimilifu</u>

## 2.5 DHANA YA UAMBISHAJI/MNYAMBULIKO (INFLECTION)

Katika Istilahi - Kiingereza - Kisuahili (1987) uambishaji umeelezwa kuwa ni:-

> "utaratibu wa kuweka viambishi katika mzizi wa neno ili kulipa maana mahususi."[11]

Kapinga (1983) anasema kuwa:

> "neno mnyambuliko linatokana na neno nyumbua au nyambua. Kunyumbua ni kurefusha kitu kama mpira. Mnyambuliko ni hali ile ya kulipa neno maana nyingine kwa kuongeza viambisho fulani fulani."12

Katika ukurasa wa 63, anaendelea kusema kwamba

> "mnyambuliko kwa jumla ni tendo la kuambatisha viambishi kwenye mizizi au mashina ya maneno ili kupata neno lenye maana ya pekee na linaloweza kupangwa kisarufi katika aina mojawapo ya maneno." 13

Tulitaja katika sehemu ya 1.3 na 1.5. kuwa baadhi ya wasomi hawatofautishi baina ya unyambuaji na uambishaji. Hya iliyonukuliwa hapo juu inathibitisha kauli hii.

Katika tasnifu hii tutachukulia uambishaji kuwa aina ya uundaji wa maneno ambapo viambisho huongezwa kwenye mzizi au msingi wa neno ili kuunda neno la kategoria ile ile. Kwa mfano mzizi wa nomino unatumiwa kuunda maneno ya kategoria ya nomino tu. Tukiwa na mzizi kama vile {ti} , tunaweza kuunda nomino kama

vile <u>Mti</u>, <u>miti</u>, <u>kiti</u>, <u>viti</u>, <u>jiti</u> n.k.

## 2.5.1. AINA ZA UAMBISHAJI

Katika uambishaji, viambisho vinavyotumika ni viambisho vitangulizi vya ngeli. Mofimu ambazo hubadilisha kitenzi kuwa nomino haziitajiki kwani hakuna kuvuka kategoria moja hadi nyingine. Katika utaratibu huu, mzizi wa nomino unavutwa ili kuleta maana au dhana tofauti. Kwa mfano dhana ya udogo au ukubwa, dhana ya umoja au wingi n.k.

mifano:

Nomino zinazoleta dhana ya umoja au wingi

{ti} → mti - miti

{tu} → mtu - watu

{to} → mto - mito

{toto} → mtoto - watoto

Nomino zinazoleta dhana ya udogo

{ti} → kijiti/vijiti

{tu} → kijitu/vijitu

{to} → kijito/vijito

{toto} → kitoto/vitoto

Dhana ya udogo huletwa kwa kutumia kiambisho {ki} katika umoja na {vi} katika wingi. Inasemekana kuwa mizizi yenye silabi <u>zisizozidi mbili</u> huunda nomino ambayo huanza kwa "kiji" au "viji" katika wingi badala

ya {ki} na {vi} (Mbaabu 1985: 122-123). Hata hivyo kuna nomino kadha kama vile <u>kijikondoo</u> na <u>kijikaratasi</u> ambanzo huchukua "kiji" na "viji" hata ingawa zina silabi zaidi ya mbili.

Kiambisho {Ki} vile vile huleta maana ya kudunisha vitu au hadhi za watu. Hivyo basi kukiongeza kiambisho hiki kwenye mizizi ya nomino hodokeza maana ya kudhahilisha na kudharau.

mifano: mu-alimu → kialimu (mwalimu mdogo)

meneja → kimeneja (meneja mdogo)

shule → kishule (shule ndogo)

shamba → kishamba (shamba dogo)

Nomino zinazoleta dhana ya hali ya ukubwa:

{ti} → jitu/majitu

{to} → jito/majito

{tu} → jitu/majitu

{toto} → toto/matoto

Hali ya ukubwa huundwa kwa kutumia {ji} katika umoja na {ma} katika wingi. Hata hivyo, nomino nyingine hazichukui kiambisho {ji} katika umoja. Nafasi ya kiambisho hiki ni kapa {Ø}. Kwa mfano

mtoto → toto/matoto

kibanda → banda/mabanda

kikombe → kombe/makombe

paka → paka/mapaka

Kiambisho [ma] cha wingi hakichukui nafasi ya [ji] bali huongezwa kwenye umbo lote la umoja. Kwa mfano tungetarajia kupata nomino matu kama wingi wa jitu lakini badala yake tunapata majitu. Viambisho [ji] na [ma] vile vile hudokeza chembe ya dharau vinapotumiwa pamoja na misingi inayosimamia binadamu. Kwa mfano neno jibaba

## 2.6 KUBADILI KATEGORIA

Neno la kategoria moja linaweza kubadilishwa ili kutumika katika kategoria nyingine. Hii hufanywa kwa kuuweka msingi katika kategoria nyingine bila kubadilisha umbo lake (Quirk, Greenbaum, Leech, Svartvik 1972). Ni utaratibu wa unyambuaji ambapo faridi fulani huwekwa katika kategoria mpya bila kuongezwa viambisho.

### 2.6.1 UTUMIAJI WA NGELI YA 15

Ngeli ya 15 ni mojawapo ya ngeli ambazo zimewahi kuzusha mijadala mingi miongoni mwa wanasarufi na wasomi wengine (Ashton 1947, Wilson 1970 n.k.). Kuhusu nomino za ngeli ya kumi na tano, Broomfield 1970 anasema yafuatayo:

> "Noun hizi zote ni majina ya matendo, na kwa asili yake ni verb. Twaweza kusema ya kuwa ni verb zinazotumika kama noun, hata zinafanya kazi ya noun" 14

Nomino zilizomo katika ngeli hii zaweza kutazamwa kwa njia mbili:

(1) Kama nomino zinazoundwa kwa kuongeza {ku} kwenye mashina ya vitenzi. Hii ina maana kuwa {ku} inatumika kama mojawapo ya mbinu za kuunda majina kutokana na vitenzi

(2) Kama vitenzi ambavyo hutumika kama nomino katika sentensi.

Wasomi kama vile Mukuriah(1987)hawakubaliani na kauli hii. Lakini sisi tunaiona kuwa na mashiko. Kwa mfano linapotajwa neno kulima au kuimba, maana inayomjia mtu ni ya kitendo cha kulima au kuimba. Lakini katika sentensi maneno haya yanaweza kutumika kama nomino.

mifano:

"Kuimba kwake kuliwapendeza wageni waliohudhuria."

"Kulima kwao kumewaletea manufaa."

Vile vile katika sentensi, maneno ya ngeli hii hutumika kama vitenzi. Kwa mfano,

(a) Ilitubidi kuandika barua kumjulisha jambo hilo

(b) Maria anapenda sana kuimba anapofanya kazi

(c) Sipendi kukimbia

Mukuriah (1987) anashikilia kuwa kando na {ku} kutumiwa kuunda nomino kutokana na mashina ya vitenzi,

mofimu hii pia "inatumika kama kiwakilishi cha jina kwenye vipande vingine mbalimbali vikiwemo vitenzi". Hatukanushi dai hili bali tunasisitiza kauli yetu kuwa maneno ya ngeli hii vilevile yanaweza kuchukuliwa kama vitenzi ambavyo vinatumika kama nomino bila ya kubadilishwa umbo. Mifano ya nomino zenye {ku} kama kiambisho kitangulizi ni

<u>kucheza</u> <u>kuzama</u> n.k.

Nomino zinazoundwa kwa njia hii hazina wingi. Imesemekana kuwa vitenzi vyote vyaweza kutumiwa kuunda nomino kwa kuongeza kiambisho {ku} cha ngeli ya kumi na tano (Mbaabu 1985). Utafiti wetu umetuelekeza kutambua ukweli wa kauli hii.

Nomino zinazoundwa kwa kutumia mofimu {ku} zaweza kuwa na kinyume chake. Kinyume hiki hupatikana kwa kuongeza /to/ baada ya {ku}. Mifano:

kuandika — kutoandika

kufagia — kutofagia

kucheza — kutocheza

kupika — kutopika

Nomino hizi pia zaweza kuwa na mofimu inayowakilisha kijina cha mtendwa.

mifano:

Ku<u>m</u>kimbia

Ku<u>w</u>apikia

Ku<u>m</u>shonea

Ku<u>m</u>tuliza

## 2.7 KIMALIZIO

Tumeona kuwa viambisho vitangulizi vya ngeli vinaweza kutumiwa kuunda nomino. Hii ni kwa kuongeza kiambisho kitangulizi kwenye msingi ambao ni kitenzi. Hali kadhalika viambisho vifuatilizi vyaweza kutumiwa kuunda nomino. Mofimu ambazo hutumiwa ni {i},{ɛ}, {o}, {fu/vu} na {ji}. Lakini viambisho vifuatilizi sharti vitumiwe pamoja na viambisho vya ngeli ili ile nomino iwe katika ngeli fulani. Viambisho vitangulizi vya ngeli vyaweza kutumiwa pekee kuunda nomino lakini viambisho vifuatilizi lazima viandamane na vya ngeli.

Kwa jumla, utumiaji wa viambisho katika kuunda nomino ni utaratibu muhimu sana. Nomino nyingi za Kiswahili zimeundwa kwa kufuatia utaratibu huu. Viambisho vitangulizi vinavyotumika zaidi katika uundaji wa nomino ni {ku}, {U}, {mu}, {ki} na {ma}. Navyo viambisho vifuatilizi vinavyounda nomino nyingi ni {i} na {o} vikifuatiwa na {ji} na mwishowe {ɛ} na {fu(vu)} ambavyo vimeunda nomino chache hadi sasa.

Mingi ya mifano tuliyotoa imetokana na mizizi na misingi ya vitenzi ambayo haijanyambuliwa. Hata hivyo, ni muhimu kutaja hapa kuwa nomino zaweza kuundwa kutokana na vitenzi ambavyo tayari vishanyambuliwa. Mifano:

patana ⟶ mapatano

patanisha → mapatanisho

kopesha → mkopeshaji

endesha → mwendeshaji

Kutokana na utafiti wetu, ni dhahiri kuwa utaratibu wa uambishaji unaunda nomino kiasi kidogo ukilinganishwa na utaratibu wa unyambuaji ambao unatoa mchango mkubwa sana.

## TANBIHI

1. TUKI, 1987 Istilahi - kiingereza - Kiswahili Ripoti ya warsh ya kanda ya utayarishaji, usanifishaji na usambazaji wa istilahi za Kiswahili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam UK 66

2. Kama 1 hapa juu lakini UK 35

3. Mbaabu, 1 (1985) Sarufi ya Kiswahili, Nairobi Kenya Publishing and Book Marketing Company Ltd. UK. 107 - 108

4. Mdee, J.S. (1986) Kiswahili: Muundo na matumizi yake: Nairobi: Intercontinental publishers Ltd. UK. 79

5. Kama 4 hapo juu lakini UK. 80

6. Kama 3 hapo juu lakini UK. 108

7. Kama 3 hapo juu lakini UK. 109

8. Kama 3 hapo juu lakini UK. 110

9. Kama 7 hapo juu

10. Kama 4 hapo juu lakini UK. 76

11. Kama 1 hapo juu lakini UK. 52

12. Kapinga, M.C., (1983) Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu. Dar-es-Salaam. TUKI UK 26

13. Kama 12 hapo juu lakini UK 63.

14. Broomfield, G.W. (1931) Sarufi ya Kiswahili London: The Sheldon press UK. 48.

# SURA YA TATU

## 3.0 NOMINO ZA MKOPO

### 3.1. UTANGULIZI

Katika tasnifu hii dhana ya 'uundaji' imetumiwa sio tu kama utaratibu wa kuunda neno kwa kutumia vipashio vya lugha hiyo hiyo bali pia kumaanisha neno lililokopwa kutoka lugha nyingine na kubadilishwa muundo ili kukubaliana na muundo wa lugha ya Kiswahili. Neno mkopo limefafanuliwa kama:-

> "neno lililochukuliwa kutoka lugha moja na kuingizwa katika lugha nyingine baada ya kufanyiwa marekebisho ili lilingane na muundo wa maneno ya lugha linakoingizwa."1

Dhana ya ukopaji imezusha mijadala mikali na migawanyiko kimaoni baina ya wasomi. Kwanza kabisa kuna wataalamu wanaodai kuwa Kiswahili hakijitoshelezi maana lazima kikope kutoka kiarabu na lugha nyingine. (Broomfield 1965, Harries, 1964). Na kunao wanaoamini kuwa Kiswahili kinaweza kuunda maneno yanayotakikana bila kutegemea ukopaji. Temu (1972) anasema:-

> "maoni yangu ni kuwa Kiswahili kinaweza kuunda maneno yote yanayohitajika kueleza yote kinachotaka katika nyanja zote"2
> (tafsiri yetu)

Kuhusu ukopaji wenyewe, baadhi ya wasomi wana maoni kuwa ikiwa Kiswahili hakina msamiati wa kutajia neno fulani, kwanza kabisa utafutwe katika lahaja zote za Kiswahili. Usipopatikana katika lahaja zote hizi basi ukopwe kutoka lugha za Kibantu.[3] Kibantu kisipotosheleza mahitaji haya ndipo tugeukie lugha nyingine za Kiafrika. Pale ambapo hatua hizi zote zinashindwa kutupa msamiati mwafaka, ndipo twende kokote kule. Naye Mdee (1986) anasema kuwa watetezi wa utohoaji wa maneno ya kigeni wanapinga utohoaji wa maneno kutoka lugha za Kiafrika kwa madai kwamba maneno haya hayasadifu kueleza dhana yanazoziwakilisha. Utohozi wa maneno ya lugha za Kiafrika unapendelewa na baadhi ya wazungumzaji kwa sababu maneno hayo yanatoa mchango unaoridhisha wa kukikuza Kiswahili ambacho ni lugha ya Kiafrika wala sio kwamba ni rahisi kueleweka kwa wazungumzaji wa lugha nyingine.

Ni jambo lisilopingika kuwa lugha nyingi za Kiafrika na hasa zile za Kibantu zina mfumo unaokaribiana sana na ule wa Kiswahili. Kukopa maneno kutoka lugha hizi husaidia kuhifadhi ule Uafrika wa Kiswahili. Hata hivyo, pale neno linapokopwa haifai kuwa ni tatizo. Chenye umuhimu ni kupata neno linalowakilisha dhana inayohitajika vilivyo. Pale neno linapokopwa hutegemea msamiati unaotakikana. Hatuwezi kutarajia kupata neno la kuwakilisha neno la Kiingereza "missile"

kutokana na lahaja za Kiswahili, Kibantu au hata lugha za Kiafrika kwa sababu hii sio dhana ya Kiafrika.

### 3.1.1. NOMINO KUTOKA LUGHA MBALIMBALI

Jamii tofauti zinapoingiliana kwa sababu yoyote ile, hapana budi kuwa na athari pande zote mbili. Mwambao wa pwani umekuwa na maingiliano mengi na wageni tofauti na athari iliyotokana na maingiliano hayo inajitokeza katika lugha (msamiati) ambayo ni kipengee kimojawapo cha utamaduni.

Kiswahili kimeathiriwa sana na Kiarabu kama msamiati wake unavyodhihirisha. Jambo hili limetiliwa nguvu na Myachina (1981) ambaye anasema kuwa zaidi ya nusu ya maneno yaliyoko katika ngeli ya tisa ni ya asili ya Kiarabu. Nomino nyingi za ngeli ya tisa hazina kiambisho kitangulizi. Ukosefu huu wa viambisho vitangulizi umeiwezesha ngeli hii kusheheni nomino nyingi zilizokopwa kutoka lugha nyingine. Kauli hii imesisitizwa na Polome (1967:101). Kimaana, mikopo kutoka Kiarabu imeenea katika nyanja nyingi sana. Kwa mfano kuna nomino za:-

(a) Kidini: mifano

| | | |
|---|---|---|
| ahera | mola | imani |
| Allah | baraka | |

(b) Biashara na usafiri wa baharini: mifano

| | |
|---|---|
| Merikebu | hesabu |
| dira | fedha |
| ramani | deni |

(c) Sheria: mifano

| | |
|---|---|
| kadhi | sheria |
| haki | talaka |

(d) Sayansi na utamaduni: mifano

| | |
|---|---|
| elimu | nahau |
| falaki | |

(e) Majina ya vitu vya kawaida kwa mfano vitu vya nyumbani, mimea n.k.

mifano : sabuni

msubili

Vile vile Kiswahili kina nomino chache zilizokopwa kutoka Kiajemi, kwa mfano

| | |
|---|---|
| bagala | teli |
| pilau | n.k. |

Kihindi, mifano:-

| | | |
|---|---|---|
| bajia | bali | dagla |
| chokora | dawati | doti |
| dengu | danzi | n.k. |

Hizi ni nomino zinazotajia vitu vya kawaida, vifaa vya kujirembesha na mimea. Kihindi vile vile kimekopwa

nomino kutoka eneo la usafiri wa baharini kwa mfano:

demani

gudi n.k.

Kutoka Kireno, Kiswahili kimekopa nomino kama vile:-

gereza bendera

bastola meza n.k.

Kituruki pia kimetoa mchango wake katika nomino kama vile <u>balozi</u> na <u>bimbashi</u>

Kutokana na Kijerumani, Kiswahili kimekopa nomino kama vile:-

daktari

misheni n.k.

Kiingereza kimechangia sana hasa katika maeneo ya utawala, sayansi na michezo. Mifano:

| | | |
|---|---|---|
| gazeti | baiskeli | motokaa |
| koloni | kampuni | komiti |
| sabmarini | eropleni | soka |

miezi kama machi, januari, disemba n.k.

Zawawi (1979) anasema kuwa maneno yaliyotambuliwa kuwa ni ya Kiajemi, Kihindi au Kireno hayakuingia katika Kiswahili moja kwa moja kutoka lugha hizi bali yaliingia kupitia Kiarabu. Hili ni swala la mjadala kwani hatuwezi kuwa na hakika kuwa msamiati huu haukuingia katika Kiswahili kutokana na wazungumzaji wa lugha

hizi wenyewe wakati wa maingiliano yao ya kibiashara au kisiasa na Waswahili.

Kiswahili hakikukopa kutoka lugha za kigeni pekee. Kimekopa kutoka lahaja nyingine za Kiswahili kwa mfano nomino 'Kisabeho' kutoka Kipemba kwa maana ya kifungua - kinywa kisicho cha majimaji.[4] Kiswahili vile vile kimekopa kutoka lugha nyingine za Kibantu na Kiafrika kwa jumla. mifano:

| | | | |
|---|---|---|---|
| * thangari | - | couchgrass | kutoka Kikikuyu (Mutahi 1986:107) |
| * moori | - | heifer | |
| * nduma | - | arrow roots | |
| Ikulu | - | StateHouse | kutoka Kinyamwezi |
| Kabwela | - | Common man | " " |
| Kitivo | - | Faculty (univ.) | " Kipare |
| Bunge | - | Parliament | " Kisukuma/ Kinyamwezi |

(Temu 1984: 118 - 119)

## 3.2. MABADILIKO YANAYOKUMBA NOMINO ZILIZOKOPWA

Katika utaratibu wa ukopaji tunachokikopa ni dhana yenyewe. Hii ina maana kuwa, ikiwa mfumo wa lugha changizi ni tofauti na ule wa lugha ya Kiswahili,

---

* mikopo hii inatumika kama maneno badala maana tayari kunayo maneno ya kuwakilisha vitu hivyo katika Kiswahili.

baada ya neno kukopwa, ni lazima lirekebishwe ili liingie katika mfumo wa Kiswahili kwa njia inayofaa. Lakini ikiwa neno lililokopwa lineshabihiana na yale ya Kiswahili kiumbo, halibadiliki. Linabakia hivyo hivyo. Kwa mfano nomino data kutokana na neno "data" la Kiingereza haibadiliki umbo.

Maneno yakisha kopwa kutoka lugha ngeni hadi Kiswahili huchukua muundo wa kifonolojia na vile vile wa kimofolojia wa Kiswahili. Nomino zilizochukua muundo wa kifonolojia wa Kiswaili ni kama vile:-

hospitali — hospital

mofimu — morpheme

televisheni — television

dainamiki — dynamics n.k.

Ili kuchukua muundo wa kimofolojia wa Kiswahili, nomino nyingine hubadilika hivi kwamba zinakuwa na mizizi mipya. Mfano mmoja wa tukio hili ni ule wa nomino madigadi iliyokopwa kutokana na "mudguard" ya Kiingereza. Nomino hii imebadiliki hivi kwamba tuna digadi kuonyesha umoja na madigadi kuonyesha wingi (Polome 1967: 176, Mutahi 1986:108). Hii inaiingiza nomino yenyewe katika

ngeli ya sita.

Nomino kama vile kitabu pia imebadilika na kuwa na mzizi tofauti. Mzizi asilia ulikuwa ni "KTB" uliokopwa kutoka Kiarabu. Wingi wa nomino hii ni vitabu. Allen (1945: 40) anasema kuwa vi- ilitumiwa kwa kudhania kimakosa kuwa ki- ni kiambisho cha Kibantu. Lakini sisi hatuchukulii tukio hili kuwa ni makosa. Tunaiona kama bahati nzuri kuwa kisadfa neno hili lilianza kwa silabi ambayo inafanana na kiambisho kitangulizi cha ngeli ya saba. Na kama ilivyo kawaida ya maneno mengine ya ngeli hii, neno hili halikuwa na budi kuchukua wingi katika ngeli ya nane. Maadam neno limeingia katika Kiswahili kwa njia inayofaa na likakubalika, haina maana kuzidi kulitizama kama tokeo la kimakosa. Isitoshe, kwa mambo kufuata mkondo huu, tumerahisishiwa kazi kwa kuondolewa tatizo la kuiainisha nomino yenyewe katika ngeli.

Mfano mwingine ni nomino duka ambayo wingi wake ni maduka. Nomino hii imetokana na mzizi wa Kiarabu "DK'N". Mzizi huu uliingia katika lugha ya Kiswahili kama dukani lakini silabi ya mwisho imechukuliwa kama kiambisho kifuatilizi ambacho si sehemu ya mzizi.

Krumm (1940) amejadili jambo hili kwa kirefu. Anasema kuwa inapotokea kuwa neno la Kiarabu linaanza kwa silabi zinazofanana na viambisho vya ngeli za Kiswahili vikiwemo ma-, mi- na ki-, wazungumzaji wa Kiswahili huchukulia silabi hizi kumaanisha ngeli. Kwa mfano ikiwa neno linaanza na ma- wazungumzaji wa Kiswahili huliweka katika ngeli ya sita na kulipa umoja katika ngeli ya tano. Kauli hii imeendelezwa zaidi na Whitely (1966) na Gregersen (1967) ambao wanamuunga mkono Krumm. Mifano wanayoitoa kutilia nguvu kauli hii ni kama vile:

| | |
|---|---|
| Mazeka<br>malaika | ngeli ya5 na 6 |
| kitabu<br>kibiriti | ngeli ya 7 na 8 |
| msumari<br>mjeledi | ngeli ya 3 na 4 |

Hata hivyo zawawi (1979) anaikanusha kauli ya Krumm. Moja kati ya sababu anazotoa kupinga kauli hii ni kuwa nomino nyingi zinazoanza kwa ma- mara nyingi huwa vile vile katika ngeli ya tisa na ya kumi. Sio katika ngeli 5 na 6 pekee. Mifano:-

| | | |
|---|---|---|
| mali | makala | |
| maiti | madini | n.k. |

Krumm (1940) anazidi kusema kuwa kando na maneno ambayo sehemu ya mzizi huchukuliwa kuwa ni kiambisho, kuna maneno mengi ya kigeni ambayo huongezwa viambisho

vya Kiswahili kwa mfano:-

sahani - Kisahani

Islamu - Kiislamu n.k.

Maneno yakisha kopwa na kuingizwa katika lugha fulani huchukua tabia za maneno mengine katika lugha hiyo pokezi. Kwa mfano nomino au vitenzi vitanyambulika kama nomino au vitenzi vingine katika lugha hiyo. Kutokana na neno la Kiingereza 'club' tunapata neno kilabu lenye wingi vilabu (ngeli ya 7 na 8). Na kutokana na neno 'dynamics' tunapata maneno yafuatayo:-

| | | |
|---|---|---|
| dainamiki | - | dynamics |
| kutodainamika | - | lacking "dynamicness" |
| dainamika | - | become dynamic |
| udainamiki | - | "dynamicness" |

Mkelle (1971) anasema kuwa baadhi ya maneno yaliyokopwa hubadilika maana baada ya kuingia katika lugha pokezi. Kwa mfano neno bazazi kutokana na 'bazzaz' neno la kiarabu lililomaanisha 'mfanya biashara wa nguo'. Lakini katika Kiswahili neno bazazi humaanisha mfanya biashara au mwenye duka anayetumia ujanja na mizungu mingine. Mswahili anaposema kuwa mtu fulani ni bazazi, ana maana kuwa mtu yule ni mjanja. Kamusi[5] ya Kiswahili sanifu inasema kwamba mtu bazazi ni yule atumiaye hila, mdanganyifu au laghai. Huenda ikawa kauli hii ya Mkelle ina mashiko kwani zawawi (1979) anasisitiza kuwa wakati mwingine maana ya neno

lililokopwa hubadilika ili neno hilo liwe sehemu mahususi ya lugha pokezi.

## 3.2.1 UNYAMBUAJI WA VITENZI VYENYE ASILI YA KIGENI

Nomino hunyambuliwa kutokana na vitenzi vilivyokopwa kutoka lugha mbalimbali za kigeni (tushazitaja lugha hizi katika sehemu ya 3.1.1). Mizizi ya vitenzi inayokopwa huwa na muundo tofauti na ile ya Kibantu. Unyambuaji wa vitenzi vya mkopo ni tofauti na ule wa vitenzi vya Kibantu (Kapinga 1983). Vitenzi vya mkopo huisnia kwa vokali tofauti kama vile /i/, /u/, /a/ na /e/ k inyume na vitenzi vya Kibantu ambavyo huishia kwa vokali /a/ pekee. Mofimu tofauti hutumiwa kuunda nomino kutokana na mizizi ya vitenzi iliyokopwa.

(a) mofimu {a}

Nomino zinazoundwa kwa kutumia mofimu hii huwa na maana tofauti tofauti kama vile matokeo ya vitendo fulani, mahali, vitu vinavyoweza kuguswa, nomino dhahania n.k. Katika utaratibu wa unyambuaji wa vitenzi viliyoazimwa, mofimu {a} huchukua mahali pa vokali ya mwisho ya kitenzi ambayo huondolewa mbali. Kama tulivyotaja awali, nomino nyingi huwa katika ngeli ya tisa na kumi kwa sababu ya kutokuwa na viambisho vitangulizi.

mifano:

fitini - fitina          faidi - faida

| | | | |
|---|---|---|---|
| fedhehi | - fedheha | bariki | - baraka |
| jeruhi | - jeraha | ghofiri | - gho i a |
| gharimu | - gharama | dhamini | - dhamana |
| ruhusu | - ruhusa | barizi | - baraza |

Nomino nyingine hazifuati mtindo huu wa kutupilia mbali vokali ya mwisho ili nafasi yake ichukuliwe na {a} . Nyingine zinafuata mtindo wa kuongeza kiambisho kitangulizi cha ngeli pamoja na mofimu {a} katika msingi wa kitenzi.

mifano:-

safiri - msafara/misafara

samehe - msamaha

ishi - maisha

hukumu - mahakama

Vile vile katika utaratibu wa kuunda nomino, vokali nyingine (zisizo za mwisho) zinabadilika.

mifano:

jeruhi - jeraha (badala ya jeruha)

Fariji - faraja (badala ya farija)

bariki - baraka " " barika)

gharimu - gharama( " " gharima)

dhuru - dhara ( " " dhura)

ajiri - ujira " " " ajira) n.k.

(b) mofimu {i}

Nomino nyingi zinazoundwa kwa kutumia {i} ni zile ambazo huishia kwa vokali hiyo hiyo. Hapa, nomino nyingi huundwa kwa kuongeza viambisho vya ngeli {mu} , {wa} na {u}. Maana ya nomino hizi hutegemea kiambisho kitangulizi kilichotumiwa.

mifano:- mtu au watu wanotenda jambo

bashiri – mbashiri/wabashiri

safari – msafiri/wasafiri

hali (ngeli ya 14)

fasidi – ufisadi

asi – uasi

(c) mofimu {o}

Nomino zinazoundwa kwa kutumia mofimu hii huwa na maana ya tokeo la jambo fulani au kitu cha kufanyia jambo fulani au hali ya kitu fulani.

mifano: matokeo (ngeli ya 5/6)

jadili – jadiliano/majadiliano

kusudi – kusudio/makusudio

kisia – kisio/makisio

jaribu – jaribio/majaribio

kitu ama vitu vya kufanyia jambo (ngeli 7 na 8)

geza – kigezo/vigezo

fidi – kifidio/vifidio

Hali (ngeli ya 14)

fusa – ufusio

fidi – ufidio

(d) mofimu {u}

Mofimu {u} hutumiwa pamoja na kiambisho cha ngeli ya kwanza na ya pili kumaanisha mtu au watu wanaotenda tendo fulani.

mifano: tii - mtiifu/watiifu
sahau - msahaulifu/wasahaulifu
dhulumu - mdhalimu/wadhalimu
kinai - mkinaifu/wakinaifu n.k.

Nomino za aina ya pili zinazoundwa kwa kutumia {u} ni zile zinazoonyesha hali.

mifano:
starehe - ustarehevu
timu - utimilifu
sahau - usahaulifu
kinai - ukinaifu

Kaitka sehemu ya (2.5.2.6) tulichagua kuita mofimu hii {fu/vu} badala ya {u} . Kwa sababu hakuna mfano wowote tulioupata ambao ulikuwa na {u} bila kuandamana na /f/ na /v/ . Lakini katika unyambuaji wa vitenzi vilivyoazimwa, tuna mifano kadha kama vile <u>mdhalimu</u>, <u>hesabu</u>, n.k.

### 3.2.2 KUBADILI KATEGORIA YA NENO

Utaratibu wa kubadili neno la Kategoria fulani ili kutumika katika kategoria nyingine hutumika miongoni mwa maneno ya mkopo. Vitenzi vilivyokopwa kutoka lugha ngeni hasa Kiarabu vinaweza kutumika kama nomino bila

kuongezwa viambisho au kubadilishwa umbo kwa njia ynyote ile. Nomino nyingi za aina hii huwa katika ngeli ya tisa na ya kumi na wakati mwingine katika ngeli ya tano na ya sita.

mifano: hukumu
fahamu
jibu
hadhari n.k.

### 3.2.3 KUFUTILIWA MBALI KWA SAUTI

Inasemekana kuwa njia nyingine ya kuunda nomino kutokana na vitenzi vilivyokopwa ni ya kutupilia mbali baadhi ya sauti zilizoko katika kitenzi chenyewe (Mbaabu 1985)

Mifano: fadhaika - fadhaa
taabika - taabu
*tahadhari - hadhari
taajabu - ajabu
takamali - kamili n.k.

Kutokana na mifano iliyoorodheshwa hapo juu tunaona vigumu kukubaliana na Mbaabu kwa sababu ni vigumu sana kujua ikiwa ni kitenzi au ni nomino iliyoazimwa na kuingizwa katika Kiswahili . Huenda ikawa ni nomino iliyoazimwa kabla ya kitenzi na kitenzi kuundwa kutokana nayo.

## 3.2.4. KUONGEZWA KWA SAUTI

Njia nyingine ya kuunda nomino kutokana na vitenzi vilivyokopwa ni ile ya kuongeza sauti kadha bila kuwa na utaratibu maalum. Kila nomino inaundwa kivyake.

mifano:

shukuru - shukrani

sawiri - taswira

laumu - lawana n.k.

* jibu - jawabu

Kando na ngumu wa kujua ikiwa ni nomino au ni kitenzi kilichokopwa kwanza, matatizo ya kuongeza au kupunguza sauti fulani yaweza kutokana na athari ya kuyaandika maneno yaliyokuwa katika hati za Kiarabu katika hati za Kilatini.

## 3.3 UTOHOZI

Utohozi ni moja katika njia maarufu sana za kukuza na kupanua msamiati wa Kiswahili. Baadhi ya wasomi akiwemo Mdee wanauita utohoaji. Mdee (1986) anasema kuwa utohoaji wa maneno ya lugha nyingine ni njia mojawapo inayotumiwa sana katika kupata istilahi

---

* maneno haya hutumika kama nomino na vile vile vitenzi. Lakini katika mifano hii tunayachukulia kuwa katika kategoria ya vitenzi.

mpya. Anaongeza kuwa utaratibu huu husaidia sana kupata istilahi wakati tunapokosa neno lifaalo kutoka lugha inayohusika.

Utohozi ni namna ya kuunda nomino hivi kwamba maneno ya lugha changizi yanafuata muundo wa lugha pokezi. Utohozi umefafanuliwa kama:-

> "utaratibu wa kubadili maunbo ya maneno yaliyokopwa ili yakubaliane na mfumo wa lugha pokezi."6

Kama tulivyotaja hapo awali (sehemu ya 3.2) neno likishakopwa hutoholewa ili likubaliwe na muundo wa maneno ya lugha pokezi kifonolojia na kimofolojia. Utaratibu wa utohozi hauwezi kuepukika kabisa. Dhana mpya iingiapo katika Kiswahili husababisha ukopaji ikiwa hakuna neno la kuisimamia. Hata hivyo, utohozi wa maneno kutoka lugha nyingine lazima ufanywe kwa makini ili Kiswahili kiweze kulifadhi sura yake.

Mara nyingi, maneno hutoholewa kwa kuzingatia matamshi ya maneno yenyewe katika lugha changizi. Kwa mfano, kutokana na neno la kiingeneza 'morphema' tunapata nomino mofimu badala ya mofemu au hata mofeme. Mifano ya maneno yaliyotoholewa ni kama vile:-

wakati - waqt (Kiarabu)

kariba - qirba "

baisikeli - bicycle (Kiingereza)

shati - shirt (Kiingereza)

shule - schule (Kijerumani)

meza - mensa (Kireno)

divai - du vin (Kifaransa) n.k.

Katika utaratibu wa kutohoa maneno, vitamkwa au sauti huongezwa pale ambapo hazikuwepo katika lugha changizi. Kwa mfano kutokana na neno la Kiingereza '<u>hospital</u>', tunapata nomino <u>hospitali</u>. Tunaona kuwa kitamkwa /i/ kimeongezwa baada ya /l/ ili kuleta muundo unaopendekezwa na Kiswahili yaani ule wa konsonanti vokali konsonanti vokali. Vile vile kuongezwa kwa kitamkwa hiki kunaliwezesha neno hili kutamkwa kama maneno mengine ya Kiswahili.

Kando na kuongezwa kwa vitamkwa katika maneno, sauti ambazo hazipatikani katika Kiswahili huondolewa na nafasi yake kuchukuliwa na sauti zinazokaribiana na hizo zilizoko katika lugha asilia. Kwa mfano Kiswahili hakina sauti /q/ na kwa hivyo nafasi yake huchukuliwa na /k/ ambayo inakaribiana nayo kimatamshi. Ndiyo maana tunapata maneno kama vile <u>wakati</u> kutokana na neno "<u>waqt</u>" na <u>kiriba</u> kutokana na neno "<u>qirba</u>" (ya Kiarabu). Maneno mengine yanayofuata mkondo huu ni kama vile:-

kudura - qudra (Kiarabu)

kaburi - qabr "

mkasi - mqaṣṣ " n.k.

Wakati mwingine baadhi ya sauti zilizoko kwenye neno asilia hutupiliwa mbali. Kwa mfano katika kuunda neno shati lililotokana na neno la Kiingereza "shirt", /r/ ilitupiliwa mbali. Katika kutohoa neno meza, kando na kuiondolea /n/ mbali, /s/ vile vile ilibadilishwa kuwa /z/.

Utohozi mara nyingine husahihisha maadishi tu. Kwa mfano inapotokea kuwa neno fulani linatamkwa sawa na vile linavyotamkwa katika lugha changizi, kinachobakia ni kulirekebisha katika maandishi. Kwa mfano:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| rula | - ruler (Kiingereza) | | |
| redio | - radio (Kiingereza) | | |
| sekta | - sector | " | |
| soka | - soccer | " | |
| baa | - bar | " | n.k. |

Mabadiliko haya yote yanatokea ili kuyafanya maneno yaliyokopwa kuchukua muundo wa silabi unaopendekezwa na Kiswahili na hivyo basi kuwa sehemu halisi ya Kiswahili. Maneno yakisha toholewa hatuwezi tena kuyaona kama ni mageni. Kwa kuyatohoa, tunayatoa ule ugeni na kuyafanya ya Kiswahili. Matamshi, muundo na tabia zinakuwa kama za manenso mengine katika Kiswahili.

Njia hii ya uundaji wa nomino ni muhimu sana kwa saba haina ubaguzi. Huyakubali maneno yoyote kutoka lugha yoyote. Neno likishakopwa kokote kule, huambatanishwa na muundo wa Kiswahili ili likubalike. Kitu cha

kuzingatia ni kuhakikisha kuwa neno linalokopwa linapewa ule mwonjo wa Kiswahili ili lisipuuzwe na wazungumzaji wa Kiswahili. Utaratibu huu wa utohozi ukafanywa kwa makini unaweza kutoa mchango mkubwa sana katika kukitajirisha kiswahili na msamiati. Maoni yetu ni kuwa hii ni mojawapo ya njia bora za kuziba mapengo yaliyomo katika Kiswahili. Isitoshe, njia yenyewe ikifuata utaratibu maalum ni rahisi kutumiwa. Wataalamu wanaopinga utohozi wanasema kuwa hakuna utaratibu maalum unaotumiwa katika kuunda istilahi hasa za taaluma za Kisayansi. Lakini katika kuunda msamiati wa kwaida, tatizo hili halipo.

Kumekuwa na madai kuwa Kiswahili bado hakijafanyiwa unchunguzi wa kutosha katika eneo hili la uundaji wa msamiati. Inasemekana kuwa neno kama 'ujamaa' linaonyesha wazi kuwa msamiati wa Kiswahili unaweza kutumika kueleza dhana mpya bila ya pingamizi (Gibbe 1983). Maoni haya ni sawa. Lakini sio kila mara ambapo neno linaweza kunyambuliwa kutokana na mizizi iliyoko katika lugha hiyo hiyo. Wakati mwingine inabidi neno likopwe na likishakopwa, utohozi umalifinyanga na kulifanya sehemu mahususi ya Kiswahili.

Utohozi unaweza kutumika katika nyanja zote za maisha. Manyumbani, maofisini, viwandani na kwinginelo wazungumzaji hupata majina mengi ya vifaa wanavyotumia

kwa kutumia utaratibu huu. Katika viwanda ambapo zana na vifaa vingi viko katika lugha za kigeni, utohozi husaidia sana kupata majina yanayoambatana na muundo wa Kiswahili. Baadhi ya vifaa vya nyumbani na vitu vya kawaida ambavyo vimepata majina kwa kutumia njia hii ni kama vile:-

| | | |
|---|---|---|
| kabati | - | cupboard (Kiingereza) |
| mkasi | - | mqass (Kiarabu) |
| mshumaa | - | mišmaa( Kiarabu) |
| ushanga | - | shanqqa (Kiarabu) |

Baadhi ya wataalamu na wasomi huona utohozi kama njia ya kuchafua lugha kwa kuweka maneno ya kigeni. Lakini kama sote tunavyojua hakuna lugha "safi" ulimwenguni. Na hata lugha ambazo husemekana kuwa zimesitawi na kujitosheleza pia zina aslimia kubwa sana ya maneno ya kigeni katika msamiati wake. Hii ni kusema kuwa kwetu sisi utohozi ni mojawapo ya njia bora za kuukuza msamiati wa Kiswahili.

## 3.4. KALEKI

Baadhi ya wasomi wanaita utaratibu huu 'tafsiri mikopo' kwa mfano Temu (1984) na Kiingi (1982). Kaleki ni ama ukopaji wa mofimu kwa maana yake au tafsiri ya mofimu kwa mofimu. Kaleki imeelezwa kuwa ni:-

"namna ya ukopaji ambapo neno lililokopwa hutafsiriwa mofimu kwa mofimu katika lugha inamoingizwa".7

Mdee (1986:123) anasema kuwa njia hii hutumiwa sana na watumiaji wa lugha wawapo katika kazi hasa katika viwanda na karakana ambapo zana zao nyingi zina majina ya kigeni. Kwa mfano:

ncha ya almasi - diamond point

rangi ya moto - reactive colour

n.k.

Ni kweli kuwa kuna baadhi ya nomino zilizoundwa kwa njia hii ambazo hutumika kirasmi katika maofisi, viwanda na sehemu nyingine za kikazi. Kwa mfano nomino kama vile:-

nguvufarasi - housepower

Taifa ripota - Nation Reporter

Likizo ya Lazima - Compulsory leave n.k.

Kando na kusaidia sana kuzalisha istilahi za sehemu hizo za kazi, njia hii inafaidi sana kwa vile inaweza kuzalisha istilahi nyingi kwa muda mfupi. Lakini hata hivyo, njia hii haipendelewi sana. Nomino nyingi zinazo undwa kwa njia hii hazitiliwi maanani sana kwa vile hazionekani kuwa na urasimu unaostahili. Nyingi huonekana kama kwamba zinachezea lugha tu. Kule kutafsiri mofimu kwa mofimu hufanya maneno yapoteze uzito yaliyokuwa nao katika lugha asilia. Na

yanapoingia katika lugha pokezi yanashindwa kuiwakilisha dhana inayokusudiwa kwa njia mwafaka. Zaidi ya hayo, tafsiri za aina hii zisipofanywa kwa makini hupotosha dhana ya msingi iliyokuwepo katika istilahi ya lugha asilia. Kwa mfano:-

ofisi ya vipimo vya Taifa - National Bureau of Standards

Sehemu ya uwenezaji - publicity section

Tafsiri hizi zinasemekana kuwa ni potofu kwa sababu hazikusawiri dhana zilizokusudiwa kama ilivyokuwa katika lugha asilia (Mdee 1986:124)

Mdee (1986) anadai kuwa istilahi zinazoundwa kwa njia hii hukubalika kwa sababu hutungwa na wajuzi wa lugha ya Kiswahili pamoja na fani wanayoishughulikia. Hili ni dai ambalo hatukubaliani nalo kwa sababu watunzi hawa huwa kamwe si wajuzi wa Kiswahili. Ni wazungumzaji wa kawaida wa kiswahili. Utaratibu huu huu unapotumiwa na wataalamu wa Kiswahili huwa ni kwa minajili ya kuchekesha kwa mfano nomino kama vile mkuu wa sakafu. Hata hivyo, utaratibu huu unatumika miongoni mwa wazungumzaji wa kawaida kwa mfano tunapata neno kama vile baba sukari kutokana na "sugar Daddy" la Kiingereza. Vile vile tunapata misemo na methali ambazo zimetafsiriwa moja kwa moja kutoka lugha n ingine hadi Kiswahili. Kwa mfano:-

rangi zinazoruka - flying colours

Damu nzito kuliko maji- blood is thicker than water

Mifano mingine ya kaleki ni kama vile:-

Likizo ya Ugonjwa - sick leave

Sekta ya kibinafsi - private sector

mama sukari - sugar mummy.

n.k.

Kaleki huwa kwa kiasi kikubwa inahusu nomino ambazo ni zaidi ya neno moja. Mara nyingi huwa ni maneno ambatano au virai (vya a- unganishi). Tafsiri zinazopatikana huwa ni ndefu ndefu na labda hii ndiyo sababu ya wazungumzaji na wataalamu wengi kutoupendelea utaratibu huu. Ni tabia ya binadamu kupendelea matamshi ya haraka haraka. Na ndiyo sababu hawapendi maneno marefu, na wakati mwingine hata huyatupilia mbali, maana hayatamkiki kwa urahisi.

## 3.5. AKRONIMU/AKRONIMI

Akronimu inaelezwa kuwa ni:-

> jina linalotokana na ufupisho wa maneno yanayotumiwa kwa pamoja kwa kuchukua herufi za mwanzo tu za maneno hayo.8

Tukizingatia muundo wa lugha ya Kiswahili kwa jumla, tunaona kuwa maelezo haya ni finyu sana. Kinyume na lugha ya Kiingereza ilivyo, ni vigumu sana kuchukua

herufi za kwanza tu za maneno ya Kiswahili na kuunda neno litakalosimamia dhana inayotakikana. Kwa mfano tukichukua kundi la maneno 'ukosefu wa kinga mwilini' na tuchukue herufi za kwanza tu, tutapara "ukm" ambalo halitatupa maana tunayoitarajia. Zaidi ya hivyo halitamkiki. Hii inaonyesha wazi kwamba ni lazima dhana hii ipanuliwe kwa kuchukua ama herufi za kwanza au silabi za kwanza au hata sehemu ya neno ili kurekebisha matamshi.

Katika Kiswahili, akronimu huundwa kwa kuchukua silabi ya kwanza, silabi mbili za mwanzo, silabi teuzi za kati au hata neno zima. Utaratibu unaofaa ni ule unaozingatia mfumo maalum. Kwa mfano ule wa kuchukua herufi au silabi za mwanzo kama katika neno ukimwi - ukosefu wa kinga mwilini. Nomino nyingine iliyoundwa kwa kufuata utaratibu huu ni huhaba - huduma hadi bandarini. Lakini maneno mengine huundwa kiholela kwa mfano chajio kutokana na chakula cha jioni. Kigezo cha utaratibu huu hakijulikani. Kwa nini chajio isiwe chajioni?

Mdee (1986) anasema kuwa njia hii haiungwi mkono sana na watumiaji wa lugha. Hii inategemea. Kuna watu wanaounga mkono na wengine wasiounga mkono. Wale wasiounga mkomo labda wanafanya hivyo kwa sababu ya njia hii kutokuwa na utaratibu maalum wa kufuatwa.

Ili ikubalike ni lazima iwe na utaratibu ulio wazi wa kuteua herufi au silabi za maneno ili kujenga neno. mifano:-

a. msikwao - mtu asiye na kwao

b. hataza - hati ya kukataza

c. fupaja - fupa la paja

d. chajio - chakula cha jioni n.k

Katika mifano iliyoko hapo juu tunaona kuwa kila neno limefuata utaratibu wake tofauti. Ili njia hii iwe na utaratibu unaokaribia kuwa rasmi tungependekeza kuwa ikiwa herufi au silabi za mwanzo mwanzo zaweza kuchukuliwa na maana inayotakikana kupatikana, basi zichukuliwe. Kwa mfano katika maneno ukimwi na huhaba, utaratibu huu umefuatwa na sehemu muhimu zimewakilishwa. Lakini katika a, c na d, mbona utaratibu tofauti utumiwe kuyapata maneno haya?

Ikiwa haiwezekani kuunda neno linalotakikana kwa kuchukua herufi au silabi za mwanzo mwanzo, basi sehemu muhimu zafaa ziorodheshwe kama ifuatavyo:-

(a) m- si kwao

(b) ha taza

(c) fupa paja

(d) cha jioni

Pale ambapo pana silabi zinzofanana, moja iondolewe kwa mfano 'fupapaja' pa- moja iondolewe. Katika mkondo huu, ikiwa neno la mwisho (ambalo mara

nyingi ndilo huwa muhimu sana) ni fupi, basi lichukuliwe .lote na utaratibu huu utakuwa rasmi. Lakini ikiwa ni ndefu kama 'kukataza' basi silabi muhimu katika neno hilo zaweza kuteuliwa. Hii itatupa nomino msikwao, hataza, fupaja na "chajioni" ambazo zitakuwa zimeundwa kwa kufuata utaratibu maalum.

Ili kuendeleza hili pendekezo letu, tutaangalia mfano wetu wenyewe wa kuunda nomino kwa kufuata hatua hizi. Tuseme kuwa tunataka kuunda neno la 'chombo cha kuzimia moto', kwanza kabisa tutateua sehemu muhimu:

cha - zima - moto

Kama tunavyojua ki- huwakilisha kifaa fulani. Kwa hivyo tunapata neno kizimamoto ambalo linaweza kufupishwa zaidi kuwa kizimoto.

Njia hii ni lazima itumiwe kwa makini ili iweze kuwakilisha dhana zinazokusudiwa kwa namna inayofaa. Jambo hili lisipozingatiwa, kutatokea vifupisho ambavyo vinatumika tu miongoni mwa makundi fulani ya watu. Kwa mfano neno Chajio ambalo lilianza na lingali linatumika kwa kiasi kikubwa miongoni mwa vijana. Maneno yaliyoundwa kwa kuzingatia utaratibu mwema kwa mfano ukimwi yanatumiwa kote na watu tofauti. Jambo lingine ambalo limelisaidia neno hili

kuenea sana ni kutangazwa sana. Neno hili linatumiwa katika taarifa ,a habari na vile vile magazetini. Maneno mengine hukosa kuwa na mizizi imara kwa vile hayakutangazwa kwa umma. Hii huyafanya kufifia kimatumizi na mwishowe kutoweka.

Njia hii inaweza kutumiwa kufupisha virai ambavyo hutumika kama nomino moja na ambavyo hutatiza mawasiliano kwa sababu ya urefu wake. Kwa mfano 'likizo ya lazima' inaweza kufanywe "Lilazima".

Utaratibu huu hutumika mara nyingi kuunda majina ya taasisi kwa mfano, TUKI - Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili. BAKITA = Baraza la Kiswahili la Taifa. Vile vile hutumiwa kuunda majina ya vyama kwa mfano, CHAKINA - Chama Cha Kiswahili Cha Chuo Kikuu Cha Naironi.

## 3.6. KIMALIZIO

Kama tulivyotaja awali, ni vigumu sana kujua ikiwa ni nomino au ni kitenzi kilichokopwa kwanza. Lakini tumechukulia kuwa ni vitenzi vilivyokopwa kwanza halafu vikanyambuliwa ili kupata nomino. Kuhusu unyambuaji wa vitenzi vilivyokopwa, tuliona kuwa {e} haitumiki kuunda nomino.

Ingawa akronimu hazihusiani moja kwa moja na ukopaji, tumeziangalia katika sehemu hii kwa sababu nyingi kati ya 'istilahi vikundi' zinazofupishwa huwa zimetokana na dhana ngeni. Zaidi ya hivyo, tunaamini kuwa utaratibu wenyewe umekopwa kutokana na lugha nyingine kama vile Kiingereza.

## TANBIHI

1. TUKI, (1987) Isitilahi - Kiingereza - Kiswahili
   Chuo Kikuu Cha Dar-es-Salaam
   UK 62.

2. Temu (1972) "Swahili vocabulary Expansion: A preliminary observation" Katika Kiswahili Vol 42/1 UK. 1

3. Tazama Chiraghdin na Mnyampala Historia ya Kiswahili, Oxford University press, Nairobi 1977. UK 64

4. Mtazame Mukhwana, A (1988) katika tasnifu ya B.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi UK. 61-62

5. TUKI, (1981) Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Oxford University press, Dar-es-Salaam.

6. Kama 1 hapo juu lakini UK.3

7. Kama 1 hapo juu lakini UK 17

8. Kama 1 hapo juu lakini UK 2

## SURA YA NNE

### 4.0 UTANGULIZI

Katika sura hii tunatizama utaratibu wa kuunganisha maneno na taratibu nyingine ndogondogo. Tunashughulikia taratibu hizi ili tuweze kuona zinatoa mchango wa kiasi gani katika uundaji wa nomino za Kiswahili.

### 4.1 MANENO AMBATANO

Maneno ambatano ni maneno mawili au zaidi yaliyounganishwa ili kuunda neno moja lenye dhana mpya. Maneno ambatano yana zaidi ya msingi au mzizi mmoja lakini hutumika kama neno moja. Maneno haya huunganishwa kuwa nomino moja na mkazo ambao hutokea kwenye silabi ya pili kutoka mwisho wa neno la pili. Silabi ya pili kutoka mwisho wa neno ya kwanza hupata mkazo hafifu sana (Polome 1967). Wakati mwingine mkazo ulioko katika neno la kwanza hupotea kabisa kama katika nomino mlariba kutokana na la + riba na chamshakinywa kutokana na amsha + kinywa.

Maneno ambatano huwa na maana ya kijumla inayohusiana na sehemu zinazoyajenga lakini isiyofahamika kwa kutazama maneno yenyewe tu. Kwa njia nyingine, maana ya neno ambatano haitabiriki kutokana na viambajengo vinavyoliunda. Katika Kiswahili maneno

ambatano huandikwa kama neno moja kwa mfano <u>kifauongo</u> au kama maneno mawili kwa mfano <u>mfanyi kazi</u>

Kapinga (1983) na (1975) anaita utaratibu huu 'mwambatano wa maneno'. Nao wataalamu wengine wanayaita vingine maneno yanayoundwa kwa njia hii kwa mfano Kiingi (1982:39) anavaita 'maneno - ungana' Naye Gibbe (1983) anayaita 'maneno pacha'. Sisi tumeamua kuyaita 'maneno ambatano' kwa sababu, kando na kuwa ndilo jina linalopendekezwa na TUKI (1987) tunaliona kuwa linafaa zaidi.

Kuhusiana na mbinu hii, Gibbe (1983) anasema kuwa kabla ya mwaka wa 1970, utaratibu huu ulitumiwa kwa nadra sana. Anazidi kueleza kuwa wataalamu wa lugha ya Kiswahili hawakuukazania wala kuuendeleza. Utaratibu huu ulijiendeleza wenyewe bila kupewa msukumo. Anaendelea kudai kuwa njia hii haijachunguzwa vizuri na kwa hivyo ingali inatumika nusunusu tu. Ili kusisitiza kauli hii, anatoa mfano wa neno <u>Elimuviumbe</u> na kusema kuwa neno hili likitazamwa kwa jicho pevu inawezekana kulifupisha zaidi na libaki linaeleweka. Linaweza kufupishwa kuwa "Eliviumbe", ambapo "Eli" itasimamia <u>elimu</u>. Lakini tukiichunguza kauli hii ya Gibbe (1983) tunaona kuwa kwa kufupisha neno <u>Elimuviumbe</u> kuwa "Eliviumbe" anaondoka katika eneo la

maneno ambatano na kuingilia eneo la uhuluti. Uhuluti ni:-

> "Kitendo cha kuviweka pamoja vipashio viwili ambavyo havipaswi kukaa pamoja kwa mujibu wa lugha hiyo katika kuunda maneno. k.v. neno chajio kutokana na chakula cha jioni"1

Mfano huu wa uhuluti unaotolewa na Taasisi ya uchunguzi hatukubaliani nao. Kwetu sisi chajio limetokana na utaratibu wa akronimi tuliouzungumzia katika sehemu ya 3.5. Uhuluti hasa ni kule kuchukua maneno mawili na kuyachanganya ili kuunda neno moja kwa mfano kutokana na maneno ya Kiingereza breakfast na lunch, neno brunch linaundwa

Tunaliondoa neno "Eliviumbe" katika kundi la maneno ambatano kwa sababu maneno ambatano huundwa kwa kuunganisha ama maneno, mizizi au misingi tofauti ili kuunda neno moja. Lakini kama tunavyojua "Eli" katika neno "Eliviumbe" sio neno wala mzizi wa neno.

Gibbe (1983) pia ametaja kuwa maneno ambatano yamekuwa yakipata mashambulizi hapa na pale. Anasema kuwa wanataaluma hawayapendelei na wanapopata istilahi nyingine huichukua mara moja. Kiingi ( 1982) anakubaliana na kauli hii na kusema kuwa wazungumzaji wa Kiswahili lazima wajifunze kukubali maneno ambatano hata ingawa ni marefu. Si ajabu kuona kuwa wazungumzaji

wa kawaida hawapendi maneno ambatano kwa sababu ni tabia ya binadamu kupendelea matamshi ya haraka. Hivyo basi kutamka neno refu kunatatiza.

Inasemekana kuwa maneno ambatano yenye asili ya Kiswahili yamekuwa yakishindana na maneno yenye asili ya kigeni. Matokeo mara nyingi yamekuwa maneno ambatano kushindwa.

| | | | |
|---|---|---|---|
| mifano: | ufundimitambo | - | uhandisi (Kiarabu) |
| | Elimuviumbe | - | biolojia (Kiingereza) |

(Gibbe 1983)

## 4.2 AINA ZA MANENO AMBATANO

Kuhusu kuunganisha maneno, Polome (1967) anasema kuwa aina moja inayotokea kwa wingi katika Kiswahili ni ile ya kuunganisha nomino iliyoundwa kutokana na mzizi wa kitenzi na yambwa tendwa ya mzizi huo. Ngeli ya maneno haya hutegemea kiambisho kitangulizi kilichotumiwa katika neno la kwanza.

mifano:

| | | |
|---|---|---|
| mwuza samaki | - | ngeli ya 1 na 2 |
| kifunga bei | - | ngeli ya 7 na 8 |
| kitinda mimba | - | " " 1 na 2 |
| mshona viatu | - | " " " " " |
| uvutaji hewa | - | " " 14 |

Nomino nyingine huundwa kwa kuunganisha <u>mfanyi</u> na vifaa kuonyesha kazi inayofanywa na wahusika kwa mfano <u>mfanyi kazi</u>, <u>mfanyi biashara</u>, n.k. Hapa

kiambajengo kinachotangulia ni kitenzi kikifuatwa na nom
Kwa upande mwingine tunaweza kuwa na nomino ikifuatwa na kitenzi.

Mifano: Jembe mzunguko - Rotovator
giasnkota - spiralgear
nyasi mchanganyiko - mixed sward
nuktatuli - fixed point n.k.

4.2.1 KUUNGANISHA NOMINO MBILI

Kiswahili pia huunda maneno kwa kuunganisha nomino mbili.

Mifano: askari kanzu
elimumwili
gugu mwitu
batamaji n.k.

Polome (1967) anasema kuwa nomino ya pili huwa na u wa kupambanua ya kwanza. Katika kundi hili, tunapata nomino nyingi ambazo zinaundwa kwa kutumia kiungo ana .

mifano: mwanachama mwanamimba
mwanachuo mwanahewa
mwanasheria mwananchi
mwanamke mwanaanga n.k.

Mara nyingi kiambajengo kinachounganishwa na {ana} huwa ni nomino. Lakini ana pia huunganishwa na nomino

zilizoundwa kutokana na mizizi ya vitenzi au vitenzi kwa mfano mwanamapinduzi, mwanafunzi na mwanandani na vile vile vivumishi kwa mfano mwanaharamu. Wakati mwingine na. hasa siku hizi , ana huunganishwa na maneno valiyokopwa kutoka lugha ngeni ili kuunda nomino za Kiswahili zinazoonyesha uhusika katika jambo au kazi fulani. Kwa mfano mwanasaikolojia na mwanakwaya.

### 4.2.2 KUUNGANISHA KIVUMISHI NA KITENZI

Nomino nyingine katika Kiswahili huundwa kwa kuunganisha kivumishi na mzizi wa kitenzi. Kwa mfano, nomino zinazoundwa kwa kutumia kivumishi kuu. Kulingana na Polome (1967) maneno yanayoundwa kwa kutumia kivumishi hiki hutumia hali iliyofupishwa yaani [ku].

mifano: mkurugenzi
mkufunzi
mkulima n.k.

Kwa upande ule mwingine nomino yaweza kuundwa kwa kuunganis mzizi wa kitenzi na kivumishi kama katika neno ujauzito.

### 4.2.3 KUUNGANISHA NOMINO NA KIVUMISHI

Nomino katika Kiswahili pia huundwa kwa kuunganisha nomino na kivumishi.

mifano: viazi vitamu
ng'ombejike
mshipa mkuu
pembenne n.k.

4.2.4 KUUNGANISHA VITENZI VIWILI

Temu (1984: 115) ametoa mfano wa neno myevungano kwa maana ya 'fusion' kwa Kiingereza kama nomino iliyoundwa kwa kuunganisha vitenzi viwili yeyusha na ungana na kutumia mofimu o kukibadilisha kitenzi kuwa nomino. Hata hivyo, njia hii haitumiki sana kuunda nomino katika Kiswahili.

4.3 TARATIBU NDOGONDOGO

Kando na taratibu muhimu tulizozishughulikia Kiswahili pia hutumia taratibu ndogondogo kadha kuunda nomino, kama tunavyozitaja punde.

4.4. URADIDI

Huu ni utaratibu wa kurejelea mzizi wa neno. Uradidi unasemekana katika mofolojia kuwa

"ni neno linalowakilisha
kurudiwarudiwa kwa
sehemu ya neno"2

Tumechukulia utaratibu huu kuwa tofauti na ule wa maneno ambatano kwa sababu katika kurejelea mzizi, ni mzizi ule ule unaorudiwa. Lakini katika kuunda maneno ambatano, neno huundwa kwa kutumia mizizi au misingi tofau

mifano:

kizunguzungu

kutangatanga

kurandaranda

chembechembe n.k.

Maneno yanayoundwa kwa kurejelea mzizi huwa na maana tofauti tofauti kama mifano iliyoko hapo juu inavyodokeza. Hata hivyo, mara nyingi urejeleaji wa mizizi hutumika kuonyesha miingo. Tanakali za sauti au neno mwigo limeelezwa kuwa ni:-

> "neno linaloiga au kuwakilisha mlio wa kitu fulani". 3

Haya ni maneno yanayoundwa na wazungumzaji wa lugha kwa kuchunguza tabia ya kitu fulani kwa mfano jinsi kinavyojiweka wa kinavyosikika. Hivyo basi hukipa jina kulingana na jinsi walivyokiona au kukisikia.

mifano: pikipiki

tingatinga

bombomu n.k.

Kapinga (1974) anasema kuwa imesemwa kwamba maneno "mama" na "baba" yameundwa kwa njia ya kuigiza sauti za watoto wanapoanza kutoa sauti kwa kupigapiga midomo na ndiyo sababu maneno hayo hupatikana katika kila lugha. Huenda dai hili likawa na mashiko kwani hata wasomi kama Quirk, Greenbaum, Leech na Svartvik (1972) wanasema kuwa mengi ya maneno ya aina hii hutokana na shule za watoto wachanga.

## 4.5 MAFUNGU YA A- UNGANISHI

Katika Kiswahili mafungu ya maneno hutumiwa sana kuunda msamiati mpya. (Myachina 1981). Mafungu haya huwa ni virai au vikundi vya a- unganishi. Kikundi cha a- unganishi huwa mara nyingi kikionyesha hali ya umilikishi. Mara nyingi vikundi hivi huundwa kwa kuzingatia maelezo au kazi inayofanywa na vifaa vyenyewe. Vikundi hivi pia huwekwa kwenye ngeli kutegemea viambisho vitangulizi vilivyotumiwa.

mifano: chombo cha kuzimia moto

mvua ya mawe

orodha ya vyakula

hati ya malipo

daftari ya fedha n.k.

## 4.6 UHAMISHAJI WA MAANA

Uhamishaji wa maana pia hutumiwa kama njia moja ya kukitajirisha Kiswahili na msamiati. Nomino huundwa kwa kuchukua neno linalokaribiana sana kimaana na dhana inayotakiwa na kulipa maana mpya. Kwa mfano neno <u>ndege</u> kwa maana ya '<u>bird</u>' kwa Kiingereza limechukua maana ya '<u>aircraft</u>'. Nalo neno <u>tawi</u> kwa maana ya '<u>branch</u>' au '<u>twig</u>' sasa limechukua maana ya '<u>section</u>' au '<u>department</u>'. Neno <u>mtego</u> hutumika katika maana yake asili kumaanisha '<u>trap</u>' kwa Kiingereza na hali kadhalika katika maana yake mpya ya '<u>mine</u>'

## 4.7. UTUMIAJI WA FONIMU ZA LUGHA

Utaratibu mwingine wa kuunda nomino unaopendekezwa ni ule wa kutumia fonimu za lugha. Mdee (1986:116) anasema kuwa uundaji wa istilahi wa nasibu, yaani kuzipangilia fonimu za lugha kulingana na utaratibu wa ujenzi wa maneno wa lugha inayohusika ili kuunda neno ambalo halipo katika lugha umependekezwa na baadhi ya wanaisimu wakiwemo Kepke (1946) na Temu (1968, 1981). Mtazamo huu unatokana na fikira kuwa binadamu wana uhuru wa kuunda maneno na kuyapa dhana, ili yaziwakilishe, jinsi wapendavyo bora tu wawe wanaafikiana kuhusu neno na dhana inayowakilishwa. Ingawa njia hii ina uwezo wa kuunda nomino nyingi ambazo hazifanani na nomino nyingine zilizo katika lugha hiyo, vile vile ingesababisha kuundwa kwa nomino ambazo hazina maana inayohusiana na dhana zinazowakilishwa nazo. Zaidi ya hayo, nomino hizi ni ngumu sana kwa wazungumzaji kuweza kudadisi maana yake iwapo hawakuhusika katika uundaji wake hasa kwa kuwa hazitokani na mzizi wa neno lolote lililo katika lugha inayohusika.

## 4.8 MATUMIZI YA KOMPYUTA

Utaratibu mwingine unaohusiana na huu (4.7) ni ule unaopendekezwa na Temu (1972). Temu (1972) anazungumza juu ya uundaji wa maneno kwa kutumia silabi za Kiswahili. Anaamini kwamba maneno mengi yanaweza kuzalishwa na

kompyuta. Katika utumiaji wa kompyuta Temu anachukulia maneno kuwa hayana maana ya kiasili. Maneno hupata maana yakianza kutumiwa. Hii inamaanisha kuwa maneno mengi yanaweza kupewa maana, na miundo mingi ambayo ilikuwa haitumiki hapo awali kuanza kutumika. Temu anakusudia kuonyesha kuwa ni asilimia ndogo sana ya maneno yanayoweza kutumika ambayo hutumika. Maneno yanayohitajika ni yale ambayo yanaafikiana na fonolojia na sarufi ya Kiswahili. Temu anasema kuwa mwanzoni istilahi hizi zitaonekana za ajabu lakini baada ya kutangazwa na kuenezwa sana, zitakubalika. Mfano mmoja alioutoa ni wa neno "sansi". Neno hili halina maana yoyote katika Kiswahili. Lakini likapewa maana ya "manufacture" kwa Kiingereza na kutangazwa, linaweza kukubalika.

Kuhusu mawazo ya Temu, Gibbe (1983) anasema:-

> "Kinadharia mawazo ya C.W. Temu
> ni mazuri lakini mawazo
> yake yamekomea mwenye
> majarida ya Taasisi ya
> Uchunguzi wa Kiswahili."4

Tunakubaliana na maoni haya ya Gibbe kwa sababu tunaona kuwa ni vigumu sana kutekeleza mawazo haya ya Temu. Kando na kuwa hadi sasa angali hajatangaza msamiati wake, ukweli usiopingika ni kwamba ni vigumu sana kutangaza na kuufanya umma uelewe msamiati wa aina hii. Unawezekana ukitangazwa neno moja moja kwa muda mrefu na hii itachukua wakati mrefu sana.

## 4.9 KUHUSISHA DHANA NA KITAJWA

Njia nyingine inayotumiwa kuunda nomino ni ile ya kuhusisha dhana na kitajwa. Njia hii huunda maneno ambayo yana maana inayohusiana na dhana inayowakilishwa ama kimaumbile, kitabia au kimatumizi. Kwa mfano tukichukua neno msichana ambalo liliundwa kibahati nasibu wakati Mswahili alipokuwa akiunda lugha yake, tunapata visawe[5] vyake kwa mfano mrembo, kisura, kipusa, n.k. Kwa namna moja au nyingine, maneno haya yanahusiana kwa njia fulani na kitajwa (msichana), Akida (1983) anasema kuwa jina la kitu fulani laweza kupatikana kwa kuleta mbinu za kutaja kitu hicho kwa kutumia sura au umbo maalum linaloonekana na kutoa taswira ambayo inafanana na kitu fulani kinachojulikana na muundaji wa msamiati mwenyewe. Wakati mwingine neno huundwa kwa kuzingatia kazi inayofanywa na kitu hicho. Kwa mfano neno makato ambalo limeundwa kutokana na kazi inayofanywa na meno yenyewe, yaani kukatia.

## 4.10 UUNDAJI WA KIBINAFSI

Nomino chache vile vile huundwa kwa kutumia utaratibu ambao tumeuita "uundaji wa kibinafsi". Wakati mwingine watu hutumia msamiati fulani kwa uzoefu tu. Wao huamua kutumia neno fulani kwa maana fulani, na watumiaji wengine wa lugha wanapolipokea neno hilo wanaliona ni nzuri na lapendeza. Hakuna anayeuliza kwa ni ugonjwa wa "pepopunda" uwe na jina hili. Pepo na punda wanahusianaje

hata waunde jina la ugonjwa huu am_ao hauhusiani kwa vyovyote na "pepo" wala "punda"? Lakini kutokana na huo uamuzi bila kushauriana, "pepopunda" limekubaliwa na hata wanaleksikografia wamelipokea na limetumiwa na kuandikwa hivyo hivyo lilivyo. Msamiati unaoundwa kwa njia hii huwa si wenye kibali cha utumizi lakini wenye vibali nao huwa hawawezi kuuzuia kwa urahisi usitumike. Hivyo basi, waweza ukafifia au ukaendelea.

## 4.11 UKATIZAJI

Utaratibu mwingine unaotumika lakini kwa nadra sana ni ule wa ukatizaji. Ukatizaji ni,

> "hatua ya kufupisha
> neno kwa kuondoa
> sehemu ya mwanzoni
> au mwishoni." 6

Katika matumizi maneno yote mawili yaani neno zima na neno mkato hutumika. Kwa mfano neno bi ambalo ni kifupisho cha ama bibi au binti.

Utaratibu huu umetokana na tabia ya binadamu kupenda maneno mafupi mafupi ili kuyatamka kwa haraka. Labda njia hii ingefaa sana kutumiwa kukata maneno ambayo ni marefu sana ili kuyafupisha na hivyo basi kurahisisha matamshi na mazungumzo kwa jumla. Hata hivyo, mara nyingine maneno yakikatwa huleta maana tofauti na ile iliyokusudiwa. Kwa mfano, katika sentensi, "yule mume alikuja hapa", neno mume halimaanishi tu mwanamume wa kawaida bali mwanamume mkubwa kwa kimo au shupavu au

anayeogopwa. Hii ina maana kuwa ikiwa utaratibu huu utatumiwa kuunda nomino sharti utumiwe kwa makini ili maana isipotoshwe.

## 4.12 KIMALIZIO

Japo maneno ambatano hayakubaliki kwa urahisi, yanazidi kuundwa na kutumika. Wakati mwingine maneno ya aina hii hayana budi kutumika kwa ukosefu wa kupata tafsiri yenye neno moja na mara nyingine inabidi kutumiwe maelezo ambayo hayawezi kufinywa kuwa neno moja.

Taratibu ambazo tumeziita 'ndogondogo' ni zile ambazo ingawa zinatumiwa kuunda nomino haziundi nomino nyingi. Vile vile baadhi ya taratibu zilizoko katika kundi hili ni mapendekezo ya baadhi ya wataalamu ambayo yangali yanasubiri kutekelezwa. Na kwa hivyo bado hayajaonyesha mazao yoyote.

TANBIHI

1. TUKI, (1987) Istilahi - Kiingereza - Kiswahili
Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam
UK. 15

2. Kama 1 hapo juu lakini UK. 80.

3. Kama 1 hapo juu lakini UK. 70

4. Gibbe, A.G. (1983) "Maendeleo ya Istilahi za Kiswahili" Katika jarida la Makala za semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili 1 Lugha ya Kiswahili: UK. 160.

5. Visawe hapa limetumiwa kwa maana ya "Synonym" katika Kiingereza.

6. Kama 1 hapo juu laikin UK. 21.

## SURA YA TANO

## 5.0 HITIMISHO

Katika sura ya kwanza (sehemu ya 1.2) tulisema kwamba tulinuia kueleza taratibu za uundaji wa nomino katika Kiswahili kwa mapana na marefu yake. Katika kuzitafiti taratibu hizi mbalimbali tulinuia kuona ni utaratibu upi unaotumika zaidi na ambao unatoa mchango mkubwa katika uundaji wa nomino,

Ili kuzitafiti taratibu zinazotumika tulizigawanya katika makundi matatu. Kundi la unyambuaji na uambishaji, kundi la tafsiri mikopo na maneno mikopo na kundi la maneno ambatano na taratibu nyingine ndogondogo. Kulingana na utafiti wetu, tuliona kuwa unyambuaji (ambao tuliutofautisha na uambishaji), ndio utaratibu unaotoa mchango mkubwa zaidi katika uundaji wa nomino za kawaida za Kiswahili. Utaratibu huu hutumia viambisho vitangulizi vya ngeli na viambisho vifuatilizi ambavyo ni mofimu za kubadilisha vitenzi kuwa nomino. Mofimu ambazo hutumiwa ni {i} ,{ɛ}, {o} , {fu/vu} na {ɟi}

Kuhusiana na utaratibu wa unyambuaji, tulijaribu kusahihisha makosa na madai yasiyo sahihi ambayo yamekuwa yakijitokeza katika tafiti za hapo awali. Tulionyesha kuwa kinyume na madai ya hapo awali nomino haziundwi kutokana na mizizi ya vitenzi pekee bali huundwa vile vile kutokana na mizizi ya kategoria

nyingine za maneno hasa vivumishi na nomino.

Vile vile tulionyesha kuwa [zi] haitumiwi kama mofimu ya kuunda nomino kutokana na mizizi ya vitenzi katika Kiswahili na kutoa sababu zake. Pia tuliona kuwa {a} hutumiwa tu katika kunyambua maneno yaliyokopwa na wala sio yenye asili ya Kibantu. Katika utafiti wetu hakuna pahala popote ambapo tulipata {n} ikitumiwa kama mofimu ya kuunda nomino.

Kuhusu unyambuaji wa vitenzi vilivyokopwa tuliona kwamba{ε}haitumiki kuundia nomino.

Katika kundi la maneno mikopo na tafsiri mikopo tuliona kuwa ni vigumu sana kujua kwa hakika ikiwa ni kitenzi au ni nomino iliyokopwa kwanza na kuingizwa katika Kiswahili. Pia tuliona kuwa utohozi unatumika sana na tukauchukulia kuwa mojawapo ya taratibu zinazofaa kwa kuongezea msamiati wa kila siku, sio tu kwa sababu ni rahisi kutumiwa na kueleweka bali kwa sababu huyafanya maneno yaliyoazimwa kuwa sehemu mahususi ya lugha ya Kiswahili.

Katika kundi la kuunganisha maneno na taratibu nyingine ndogondogo, tuliona kuwa hizi ni taratibu ambazo hazitumiwi sana kuunda nomino. Hii ni kusema kuwa nyingi kati ya hizi zimetumiwa tu kuunda nomino chache sana.

Kuhusu mapendekezo ya baadhi ya wataalamu kwa mfano, utumiaji wa kompyuta (Temu) tuna maoni kuwa ingawa njia hii ingezalisha nomino nyingi, ina matatizo mengi yanayohusiana na kuzitangaza nomino hizo. Hivyo basi, hii ni njia ambayo, kando na ugumu wa kueleweka na umma, ingechukua muda mrefu ikizitangaza hizo nomino.

Pendekezo letu ni kuwa iwapo kuna pengo fulani la msamiati katika mawasiliano ya kawaida, basi utaratibu wa unyambuaji utumiwe. Na iwapo hili haliwezekani basi utohozi utumiwe. Hii ni kwa sababu hizi ni taratibu ambazo ni rahisi kueleweka na umma. Unyambuaji hutumia mizizi ambayo mara nyingi huwa inajulikana na watumiaji wa lugha hiyo na utohozi hueleweka kwa urahisi kwa sababu ya kule kufanana kidogo na neno la asili. Taratibu zilizosalia zikitumiwa nomimo zilizoundwa kutokana nazo sharti zitangazwe ili zieleweke na umma.

MAREJEO

Akida, H. (1971) "Msamiati wa Muda wa Sayansi (Elimuviumbe)" Katika jarida la Kiswahili Vol. 41/1:8

__________(1971) "Msamiati wa biology - Elimuviumbe (wa muda tu)" Katika jarida la Kiswahili Vol 41/2:95

__________(1973) "Msamiati wa Elimuviumbe" katika jarida la Kiswahili Vol. 43/2:116

__________(1975) "Msamiati wa Muda Wa Elimuviumbe" Katika jarida la Kiswahili Vol. 45/1:57

__________(1983) "Ukuzaji na uendelezaji wa msamiati wa Kiswahili" Katika jarida la Makala za semina ya kimataifa ya waandishi wa Kiswahili 1 lugha ya Kiswahili: 113

Allen, J.W.T. (1945) Arabic Script for Students of Swahili: Published for the editorial Committee Tanganyika Notes and Records.

Ali, M. (1965) "Matatizo na matatuzi ya kutafsiri Sheria" Katika jarida la Kiswahili Vol. 35/1:

Archbold, M. (1973) "Msamiati wa Elimuviumbe (biological terms" Katika jarida la Kiswahili Vol.43/2:113 Taasisi ya uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dar-es-Salaam.

Ashton, E.O. (1944) Swahili Grammar, London: Longman.

Besha, R (1977) "Somo la sarufi ya lugha kwa kidato cha tano na cha sita" Katika jarida la Mulika 3:

Burt, F. (1910) Swahili Grammar and Vocabulary London: S.P.C.K.

Gibbe, A.G. (1983) "Maendeleo ya istilahi za Kiswahili" Katika jarida la Makala za semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili 1 lugha ya Kiswahili: 144.

Gregersen, E.A. (1967) Prefix ans pronoun in Bantu publications in Anthropology and Linguistics, Memoir 21, Vol. 33 no.3 Bloomington, Indian: Indian University press.

Gurnah, A.M. (1974) "Agricultural terms in Kiswahili: Msamiati wa Elimu ya Ukulima" Katika jarida la Kiswahili Vol 44/2 :32

Hooper J.B. (1976) An introduction to Natural Generative phonology. New York: Academic press.

Hyder, M (1965) "Swahili in the technical Age" katika Contemporary African Monographs. Nairobi: WE.A. Academy.

Johnson, F (1939) A standard swahili Dictionary. The inter-Territorial Language Committee. Oxford University press.

__________ (1955) Kamusi ya Kiswahili: London. The Sheldon press

Kapinga, C. (1975) "Maneno yanayofanya msamiati wa Kiswahili" katika jarida la Mulika 7: 44

Kapinga, M.C. (1983) sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu. Dar es Salaam. TUKI

Kiimbila, J.K (1971) "Uchunguzi wa maneno ya kisiasa" Katika jarida ya Kiswahili Vol 41/2

Kiingi, K.B. (1982) "Maneno ya kukopa na tafsiri za kukopa katika Kiswahili Cha kisayansi na kitekinolojia" katika jarida la Mwamko toleo la kwanza. Jarida la chama cha Kiswahili cha Chuo Kikuu cha Nairobi: 38

Kiingi, K.B. (1984) "Some Obstacles to the vocabulary Expansion of Scientific Kiswahili" katika jarida la Mwamko toleo la pili:79.

____________ (1987) "Biological nomeclature"katika jarida la Mwamko tokeo la 4:1

Knappert, J. (1962/3) "Derivation of Nouns of Action in -O in Swahili" katika jarida la Kiswahili Vol 33:

Krumm, B. (1932, 1940) Words of Oriental Language in Swahili: London

Madalia, A (1972) "Mechanical Engineering Terminology" katika jarida la Kiswahili Vol 42/1:

Mbaabu, I (1985) Sarufi ya Kiswahili: Nairobi: Kenya publishing and Book marketing Co. Ltd.

Mbunda, F.L. (1976) "Kiswahili na mfumo wake III - nomino" Katika jarida la Kioo Cha lugha toleo la 4 na 5:12

Mdee J.S. (1986) "Matatizo ya kuunda istilahi kama yanavyojitokeza katika Kiswahili" Katika jarida la Kiswahili Vol 53/1/ na 2:115

____________ (1986) Kiswahili - muundo na matumizi yake: Nairobi. Intercontinental publishers Ltd.

Mkelle, M.B. (1971) "Change in content and meaning of words" Katika jarida la Kiswahili Vol 41/1:100

Mutahi, E.K. (1986) "Swahili Lexical Expansion - prospects and problems" Katika jarida la Kiswahili Vol 53/1 na 2:104

Myachina, E.N. (1981) The swahili Language, London: Routledge and Kegan Paul.

Mzuzuri, U.D. (1974) "Msamiati wa Muda wa Chuo Cha TANU Kivukoni" Katika jarida la Kiswahili Vol 44/1:67

Njoroge, D.N. (1978) "Kikuyu deverbatives and other nominalizations" Tasnifu ya M.A. Unpublished.

Omari, C.K. (1969) "Towards the development of Kiswahili theological terms" Katika jarida la Kiswahili Vol 39:

Polome, E (1967) Swahili Language Handbook Washington DC: Center for Applied Linguistics

Quirk, R. Greenbaum, S. Leech, G. Svartvik, J. (1972) A grammar of contemporary English. London: Longman.

Ruhumbika, G. (1983) "Tafsiri za maandishi ya Kigeni kwa Kiswahili" Katika jarida la Makala za semina ya kimataifa ya waandishi wa Kiswahili II uandishi na Uchapishaji Dar es Salaam. TUKI:83

Rzewuski, E.(1975) "Phonetic structure of swahili nominal roots" Katika jarida la Kiswahili Vol 45/1:10

Temu, C.W. (1972) "Swahili vocabularly Expansion. A preliminary observation" Katika jarida la Kiswahili Vol 42/1:1

___________(1984) "Kiswahili terminology: principles adopted for the Enrichment of the Kiswahili Language" Katika jarida la Kiswahili Vol 51/1:112

Temu, C.W. (1974) "Swahili Phonetical word Building Resources" Katika jarida la Kiswahili Vol 44/1:8

Trager, L. (1973) "Formation of nouns from verbs in swahili" Katika jarida la Kiswahili Vol 42/2, 43/1:28

TUKI, (1981) Kamusi ya Kiswahili sanifu (A standard Swahili - Swahili Dictionary) Dar es Salaam: Oxford University Press.

______(1987) Istilahi - Kiingereza - Kiswahili Ripoti ya warsha ya kanda ya utayarishaji, usanifishaji na usambazaji wa istilahi za Kiswahili: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Weston, P (1965) "Law in Swahili - problems in Developing The National Language" Katika jarida la Kiswahili Vol 35/2: TUKI

Whiteley, W.H. (1967) "Swahili Nominal classes and English Loan words: A preliminary Survey" Actes du colloque International sur la classification nominale dans les langues Negro-africaines, Aix - en - provence, 3-7 July 1967: Paris:157-174.

Zawawi, S.M. (1979) Loan words and their effect on classification of swahili nominals: Leiden: E.J. Brill.